SportPesa
TZS. 783,781,040
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SHAHIDI** aeleza mgawo mil. 90/- kesi ya Sabaya




UKURASA 11

Jumamosi Desemba 18, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580798
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# WAMEUMIZA VICHWA

**WADAU** wa siasa waliojifungia siku tatu waibuka na mambo 80, limo la Katiba Mpya ...*Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 4

## WAZIRI: MARUFUKU KUFUTA LIKIZO ZA WATUMISHI



WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed...

UKURASA WA 4

## LUKUVI ATAJA KIINI MIGOGORO YA ARDHI

WAKATI Mkoa wa Dar es Salaam ukitajwa kuwa kitovu cha migogoro ya ardhi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William...

UKURASA WA 7

## MBARAWA AIBUA MADUDU UJENZI JENGO LA ABIRIA UWANJA WA NDEGE

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amegundua kasoro katika ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa...



RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi akihutubia katika hafla ya ufungaji wa Mkutano wa Wadau wa Kujadili hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Nchini Tanzania, uliowashirikisha Viongozi mbalimbali wa Vyama vya Siasa Tanzania uliofanyika katika ukumbi wa Hazina Jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Polepole apigwa 'nyundo' na TCRA

UKURASA 3

## Samia aibua shangwe, nderemo kwa walimu

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA, KAGERA KIBARUANI BARA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk Doroth Gwajima (katikati) akiwakabidhi Jackline Silemu (watatu kutoka kushoto) na mpigapicha wake Peter Rogers (wakwanza kushoto ) tuzo ya waandishi bora wa habari za afya na mazingira 2021 kundi la runinga tuzo hizo zilikabidhiwa jana Jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wameumiza vichwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAMEUMIZA vichwa! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na kilichojiri kwenye mkutano wa wadau wa siasa waliokuwa jijini Dodoma kujadili hali ya demokrasia ya vyama vingi nchini.

Wadau hao walioshiriki mkutano huo wa siku tatu kuyajadili masuala hayo, wamebainisha mambo 80 yanayohitaji kufanyiwa kazi ikiwamo marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Polisi ili kuondoa vitendo vya uonevu kwa wanasisa nchini.

Mwenyekiti wa mkutano wa wadau hao, Prof. Rwekaza Mukandala, alibainisha hayo jana alipowasilisha kilichobainishwa na wadau hao katika mkutano wa kujadili hali ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

Alisema katika kongamao hilo wadau walibainisha masuala 80 na kati ya hayo ni umuhimu wa mkutano kama huo kwa wadau wa masuala ya siasa ya vyama vingi nchini.

"Mkutano huu ni muhimu na tudumishe utaratibu wa kukutana mara kwa mara ili kutatua changamoto zetu kwa njia ya mazungumzo," Prof. Mukandala alisema.

Alibainisha jambo lingine lililowasilishwa katika mkutano huo ni umuhimu wa wadau wa siasa kufuata katiba, sheria, kanuni na miongozo katika kutekeleza majukumu yao.

Alisema vyombo vya uamuzi navyo vinapaswa kutenda haki na kulinda amani kwa kuwa msingi wa amani ni haki.

"Vyama vya siasa vitoe nafasi maalumu kwa makundi hususani wanawake na walemavu kwa kuwa michango yao ni muhimu na demokrasia inategemea mazingira ya nchi husika, uchumi, tamaduni, mila na desturi za nchi, hivyo tusiwe watu wa kuiga demokrasia za nchi nyingine," alisema.

Prof. Mukandala pia alisema elimu ya uraia iwe endelevu na ianzie ngazi ya chekechea na isisubiri wakati wa uchaguzi.

Alisema serikali na vyombo vya dola vinapaswa kuepuka upendeleo vinapohudumia vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla.

"Sheria ya Vyama vya Siasa ifanyiwe mapitio upya na mchakato uwe shirikishi. Sheria ya Polisi ifanyiwe mapitio yatakayofanya jeshi hilo kuwa na weledi na kuondoa uonevu unaofanywa na jeshi hilo kwa kisingizio cha kutekeleza sheria," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema jambo lingine lililowasilishwa kwenye mkutano huo ni viongozi wa siasa wawe na hofu ya Mungu katika utendaji wa kazi zao na kuwa waadilifu, watii sheria na wazalendo na uchungu wa kulinda amani ya nchi.

"Sote tunasafiri kwa jahazi moja likitobolewa tunazama wote," Prof. Mukandala alionya.

Vilevile, alisema malalamiko ya wananchi na wadau yanapaswa kushughulikiwa mapema pasipo kusubiri shida ijitokeze.

**MIKUTANO, KATIBA MPYA**

Alisema mikutano ya hadhara ni haki ya vyama vya siasa, hivyo visizuiliwe bali utengenezwe utaratibu wa kutoa adhabu kwa chama ambacho kitaonekana kuvunja utaratibu huo.

Prof. Mukandala pia alisema washiriki wanapendekeza badala ya kuendelea na mchakato wa Katiba Mpya, ni vyema kuchagua mambo machache yanayolalamikiwa kwa kiwango kikubwa na kuanza nayo ili kuepuka kurudia mchakato mzima.

"Rushwa za uchaguzi pia ni tatizo ambalo tunapaswa kulifanyia kazi kwa umakini," Mwenyekiti huyo aliwasilisha sehemu ya mambo 80 yaliyotiliwa mkazo.

Rais wa Zanzibar, Dk. Husein Ali Mwinyi, alisema serikali zote mbili zimeyachukua mambo hayo na zitakwenda kuyafanyia kazi kwa maslahi ya nchi.

Awali, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Vijana, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema watahakikisha Tanzania inakuwa nchi ya mfano katika masuala ya demkrasia duniani.

# Gwajima, Polepole waitwa kuhojiwa Kamati Kuu CCM

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Taifa imeazimia kuwaita Jerry Silaa, Askofu Josephat Gwajima na Humphrey Polepole ili kuwasikiliza baada ya kujadili taarifa kuhusu mwenendo wao.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana jioni na Shaka Hamdu Shaka, Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Itikadi na Uenezi, kamati hiyo ilikutana jana chini ya Mwenyekiti wa chama hicho na Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

Alisema kuwa pamoja na mambo mengine, kamati hiyo ilipokea na kujadili taarifa za mwenendo wa wanachama na viongozi wake hao watatu.

"Baada ya kuzingatia kwa kina taarifa hiyo, Kamati Kuu imeazimia kuwaita viongozi hao, ili kuwapa fursa ya kuwasikiliza kama inavyoagizwa na Kanuni za Uongozi na Maadili, Toleo la Mwaka 2017 na Katiba ya CCM ya Mwaka 1977, Toleo la 2020," Shaka alisema katika taarifa yake hiyo.

# Samia aibua shangwe, nderemo kwa walimu

**Na Joseph Mwendapole**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema anazifahamu kero za walimu na atazifanyia kazi huku akiwapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya.

Alitoa ahadi hiyo jana alipozungumza nao kwa njia ya simu kwenye ufungaji wa mkutano wa wakuu wa shule za sekondari uliofanyika Mlimani City mkoani Dar es Salaam.

Mkutano huo wa siku tatu uliratibiwa na Global Education Link (GEL) na Umoja wa Walimu wa Shule za Sekondari (TAHOSSA), kauli hiyo ya Rais Samia ikiibua shangwe na nderemo kwa washiriki waliokuwa ukumbini.

Rais Samia alimpigia simu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye ufungaji wa mkutano huo.

Mkuu wa Nchi alisema alipanga kuhudhuria mkutano huo lakini hakufanikiwa kutokana na majukumu makubwa aliyonayo.

"Ilikuwa niwe na nyinyi lakini sikuweza kutokana na kutingwa na majukumu, ninatambua 'issues' zenu, nitazifanyia kazi, " alisema Rais Samia na kusababisha walimu 'kulipuka' kwa furaha.

Mbali na hayo, Rais Samia alisema anatambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa na walimu na aliwapongeza huku akiwataka waendelee kuchapa kazi.

Rais Samia aliwahakikishia walimu hao wakiwamo viongozi wa chama chao (TAHOSSA) ambao aliwataja kwa majina kuwa serikali itaendelea kumaliza kero zinazowakabili.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Prof. Ndalichako aliwataka walimu wazingatie miongozo wanapotoa adhabu kwa wanafunzi.

Alisema baadhi ya walimu wamekuwa wakitoa adhabu kinyume cha miongozo na taratibu, kiasi cha kuwafanya wanafunzi kuchukia shule.

Waziri huyo alisema baadhi ya shule zimekuwa zikiwakatalia wanafunzi kwenda likizo kwa kisingizio cha masomo ya ziada na kuwalazimisha kulipia masomo hayo.

Alisema amekuwa akipata malalamiko mengi kutoka kwa wazazi kuwa wanafunzi huzuiwa kwenda nyumbani wakati wa likizo.

Prof. Ndalichako alisema likizo ni haki ya msingi ya mwanafunzi kwa kuwa anahitaji mapumziko ya kutembelea ndugu jamaa na marafiki na kama kuna ulazima wa masomo ya ziada, wapate kibali kutoka kwa maofisa elimu.

"Tusigeuze shule kuwa magereza, yaani mwanafunzi akianza kidato cha kwanza harudi nyumbani hadi kidato cha nne, hapana! Sote tumesoma na tunakumbuka tulivyokuwa tunarudi nyumbani likizo," alisema.

## HABARI KITAIFA



Fundi akijenga kingo kwa ajili ya kutenganisha barabara ya mabasi ya mwendokasi na magari mengine, eneo la Kimara Stop Over jijini Dar es Salaam jana **PICHA: SABATO KASIKA**

# Polepole apigwa 'nyundo' TCRA

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imekisimamisha kwa muda usiojulikana kipindi cha Shule ya Uongozi cha Televisheni ya Mtandaoni, kwa makosa matatu likiwamo la kutoa taarifa ya upotoshaji kuhusu chanjo ya corona.

Kipindi hicho kinachomilikiwa na Mbunge wa Kuteuliwa, Humphrey Polepole, pia kimekutwa na makosa ya kutoa maneno ya uongo na udhalilishaji kuwa viongozi wengi waliopo katika serikali ya awamu ya sita ni waoga kusema ukweli kuhusu deni la taifa.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui ya TCRA, Hans Gunze, alisema kosa lingine lililofanywa na kipindi hicho ni kusema viongozi wa mikoa hawajafuata utaratibu wa kuwahamisha machinga ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha badala yake ilikuwa dhuluma na unyanyasaji.

"Kamati ya maudhui imeridhia pasipokuwa na shaka kuwa Humphrey Polepole kupitia vipindi vyake tajwa, amekiuka kanuni za mawasiliano ya kieletroniki na posta katika kurusha maudhui ya mtandaoni.

"Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 44 kifungu cha pili kidogo na sehemu ya G cha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania sura ya 172,"alisema. Gunze alisema kutokana na makosa hayo, kamati imeamua kuwa kituo chake kizingatie sheria na kanuni za utangazaji ikiwa ni pamoja na kuwa na watendaji wenye weledi na taaluma ya uandishi wa habari na kuchagua maneno yenye staha . Alisema kituo hicho kikitimiza masharti hayo, mmiliki atapaswa kutoa taarifa TCRA na baada ya kuzingatia maelekezo hayo, kitakuwa katika uangalizi chini ya TCRA kwa muda wa miezi sita.

Gunze aliongeza kuwa mmiliki wa kituo hicho anayo haki ya kukata rufani ndani ya siku 21 dhidi ya uamuzi huo katika Baraza la Ushindani la Haki ya Kibiashara (FCT).

Polepole kwa upande wake aliishukuru Kamati ya Maudhui ya TCRA na kusema kuwa kazi ya kusema ukweli ina safari ndefu, hivyo hatakata tamaa katika kuendelea kusema ukweli.

Alisema kituo chake kufungiwa anaamini ni mtihani mdogo na uamuzi uliotolewa na TCRA atautafakari. "Kazi ya kusema ukweli ina safari kidogo kwa mimi ambaye ni mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ninaeamini katika kusema ukweli daima bila kuweka chembe ya fitina," alisema Polepole.

Wakati huo huo, Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, inatarajiwa kukutana leo kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali.

Moja ya mambo ambayo yanadhaniwa kutolewa uamuzi ni suala la Polepole kuendelea kuisema vibaya serikali kupitia kipindi chake cha Shule ya Uongozi, kabla hakijafungiwa.

Polepole aliyewahi kuwa Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi CCM Taifa, katika siku za hivi karibuni amekuwa akionekana kwenda kinyume cha mweleke o wa chama hicho na serikali.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa nchini, wanasema huenda mkutano wa leo ambao unaongozwa na Mwenyekiti wake, Rais Samia Suluhu Hassan, ukampa adhabu.

Mkutano huo ulitanguliwa na vikao vya Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa na Sekretarieti ya Halmashauri Kuu, vilivyoanza Desemba 15 na kukamilika leo.

# Shahidi aeleza mgawo wa mil. 90/- kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

OFISA Uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(TAKUKURU), Ramadhani Juma (39), ameeleza mahakamani mchanganuo wa mgawanyo wa Sh. milioni 90 zinazodaiwa kuchukuliwa kwa mfanyabiashara Francis Mroso.

Shahidi huyo wa 13 wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita , alidai hayo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, mbele ya Hakimu Mkazi Patricia Kisinda, wakati akiendelea na ushahidi wake.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Sylvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31). Alidai kwamba fedha hizo alikabidhiwa Sabaya na kijana wake wakiwa katika eneo la AIM MALL, Majengo jijini Arusha.

Alidai kwamba Sabaya alipewa fedha hizo kwa kumlazimisha mfanyabiashara Francis Mroso na alipokabidhiwa aliziingiza katika gari la Serikali lenye namba za usajili STL 5434. Baada ya hapo, alidai kuwa walikwenda kula maisha na vijana wake katika Hoteli ya Tulia Lodge, Sakina jijini hapa.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, Juma alidai kwamba baada ya Sabaya kukabidhiwa fedha hizo, aliwagawia vijana wake.

"Baada ya kazi mgawo ulikuwa hivi; John Odemba Sh. 300,000, Sadick Kiiza 400,000, Nathan Msuya Sh. 500,000, Watson Sh. 600,000, Enock Togolani Sh. milioni 1.5, Sylvester Nyegu Sh. milioni 2.2 na Jakson Macha Sh. milioni 1.4," alidai.

Shahidi huyo alidai kwamba baada ya kupata fedha hizo wakiwa Tulia Lodge, walikunywa na kula vyakula ndipo alipowagawia fedha hizo.

Alidai kuwa kupitia kamera za CCTV za benki ya CRDB tawi la Kwa Murombo, vijana wa Sabaya, walipatiwa Sh. milioni 90 na Mroso na kwamba walibaini kupitia kamera hizo kwamba vijana hao, walimweka chini ya ulinzi Mroso wakati akiendelea kutoa fedha benki.

Pia alidai kuwa June Mosi, mwaka huu, alianza kufanya uchambuzi wa vielelezo zikiwamo video za kamera za CCTV ambazo zilikuwa zikionyesha vijana wa Sabaya wakikabidhiwa fedha benki.

Katika kuchambua vielelezo hivyo, alidai kuwa alibaini kwamba Mroso alikuwa akimiliki akaunti katika benki hiyo na kwamba kupitia akaunti ya mfanyabiashara huyo, Januari 22, alitoa Sh. milioni 90.

Aidha, kupitia video hizo, alidai kubaini kwamba Macha na Togolani, walionekana wakiwa benki na Mroso wakati akitoa fedha hizo na kwamba wakati mfanyabiashara huyo akiendelea na utaratibu wa kutoa fedha hizo, vijana hao walimweka chini ya ulinzi kwa kuwa kila sehemu aliyokuwa akienda benki walimfuata na walimzuia kuzungumza na simu. "Mroso alipewa Sh. milioni 90 benki zilizokuwa kwenye boksi na Macha alikuwa akishuhudia makabidhiano hayo. Baada ya hapo, walibeba fedha hizo na kuingia katika gari la mfanyabiashara huyo na kuondoka katika eneo hilo," alidai Juma. Shahidi pia alidai katika uchunguzi wake, alibaini kwamba Sabaya alipewa fedha hizo baada ya kumlazimisha Mroso. Kuhusu mgawo wa fedha, alidai kuubaini kupitia taarifa fiche na baada ya kuwahoji, washtakiwa walikiri kupata mgawo.

Mawakili wa utetezi wakiongozwa na Edmund Ngemela, walipinga kitendo ya shahidi huyo kuizungumzia video ya CCTV wakidai kwamba hakuhusika kuiandaa.

**HATA HIVYO,**

Wakili Kwetukia alipinga kwa kudai kuwa shahidi huyo ni mhusika katika kuielezea video hiyo kwa kuwa ndiyo mpelelezi mkuu wa kesi hiyo. Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, Hakimu Kisinda aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 29, mwaka huu, wakati mahakama hiyo itakapotoa uamuzi mdogo

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA-MWANZA**
**SHAURI NO. 30 LA 2021**

1. **ISMAIL WAIS**
2. **MAMILE MTEBE**
3. **WILLIAM M. MTEBE**
4. **JULIET MAWADRI**

} ……………………..**WALETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **GABRIEL MAZIKU**
2. **MARK SHIFAYA URASA**
3. **NYITWA GODFREY**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: MARK SHIFAYA NA NYITWA GODFREY**

Unafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 15/03/2022 katika Chumba cha Baraza, Jengo liko Mkabala na Mahakama ya Mwanzo mjini - Nyamagana.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.
KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 14/12/2021.

**MURIRYA N.**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**MWANZA**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**CATHERINE OSCAR MICHAEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0256/0005** kilichotolewa Baraza na Mitihani la Taifa kupitia **HURUMA GIRLS SEKONDARI** mwaka 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/587600/2021.**

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**CHARLES EVARIST SIMBA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA I S T YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 226 CXK**. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI: **KAH/RB/TR/ 403/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA 41 YA 2021**
**JUDE JOHN MASHAM msimamizi wa mirathi ya marehemu ZAINABU KANYAKA LOKU**
**……………..…………..…MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**TANZANIA FERTILIZERS CO LIMITED**
**ELIKUNDA JOHN MASHAM**
**KAPONDOGORO AUCTION MARTH CO LTD……………..WAJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**TANZANIA FERTILIZERS CO LIMITED**
**ELIKUNDA JOHN MASHAM**
**KAPONDOGORO AUCTION MART CO LTD**

Popote mlipo mnaarifiwa mfike katika baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro **tarehe 20/12/2021** mbele ya Mwenyekiti M.khassim nyinyi mwenyewe binafsi au mtume muwakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa .Endapo hamtahudhulia maombi yatatajwa na kusikiliwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa **MKONO** wangu ba MUHURI wa Baraza leo **tarehe 30 Mwezi November 2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBA ……216….2018**
**MSIMAMIZI (1) Noah Mwakafwila(2)Miriam Mohamed**
**Kwa:Noah Mwakafwila**
**Mbeya**
**Msimamizi:Mariam Mohamed**
**Madai ya Mirathi.**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikiliwa mnamo tarehe 07 mwezi 01 mwaka 2022 saa8:30 asubuhi

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 12 mwaka 2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**FORM II**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya Wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa wa TANGA**

**Usimamizi wa mirathi NA. 220/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ROGER'S REGINALD MWAVYA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA STEPHEN REGINALD MWAVYA**

**TANGAZO**

*(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 7 Mwezi 01 Mwaka 2022 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia: Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 17 Mwezi 12 Mwaka 2021.

HABARI KITAIFA

# Waziri: Marufuku kufuta likizo za watumishi

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amepiga marufuku uzuiaji holela wa likizo za watumishi wa umma.

Amesema likizo ni haki ya mtumishi kisheria, hivyo hakuna haja ya kiongozi kuzuia haki hiyo isipokuwa kwa sababu maalumu ambayo mtumishi husika atashirikishwa.

Mchengerwa aliyasema hayo jana mjini hapa wakati wa ziara yake ya kikazi ya kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma na kukagua utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mkoani Geita. Alisisitiza kuwa kiongozi anapotaka kuzuia likizo ya mtumishi hana budi kufuata taratibu ambazo ni pamoja na kuzungumza na mtumishi husika anayetaka kuchukua likizo ama kwa kumlipa gharama za kuzuia likizo au kumsogezea muda.

Waziri aliwataka viongozi kuwa na utamaduni wa kusoma nyaraka mbalimbali za kiutumishi ili kujua sheria na taratibu zitakazowasaidia kuwaongoza pale wanapotaka kutoa matamko yanayozuia stahiki za mtumishi.

Alisema ni vizuri kuzungumza na mtumishi kwa kutumia lugha nzuri na akaelewa kuliko kutumia cheo, nafasi au lugha kali kwa kuwa inaweza kusababisha mtu asifanye kazi inavyotakiwa.

"Sisi viongozi tujitahidi sana kujenga matumaini kwenye mioyo ya watumishi tunaowaongoza. Tuwasikilize na kutatua kero zao, tuwe karibu nao ili wasiwe waoga na hatimaye kupoteza ubunifu walio nao katika utendaji kazi wao," alisisitiza.

Katika kusisitiza maelekezo yake, Mchengerwa alisema yeye ndiye Waziri anayesimamia masuala ya utumishi wa umma na utawala bora, hivyo ni lazima ahakikishe haki za watumishi zinapatikana kwani kama atashindwa kufanya hivyo, atakuwa hana sababu ya kuwepo kwenye wadhifa huo.

Mchengerwa yuko kwenye ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani Geita.

Kwa miaka kadhaa, baadhi ya viongozi wakiwamo wakuu wa mikoa wamekuwa wakitangaza kufuta au kuzuia likizo za watumishi wa umma kwa madai ya kusimamia shughuli mbalimbali ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Hivi karibuni kwa mfano, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitangaza kufuta likizo kwa watumishi wote wa serikali ambao idara zao zinahusika na ujenzi wa miradi ya miundombinu, vyumba vya madarasa na madawati.

Homera alitangaza hilo Jumanne wiki hii katika kata ya Mwakibete alipotembelea chanzo cha maji cha Nzovwe kinachosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya huku akibainisha kufuta likizo kwa wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri zote, maofisa ununuzi, watendaji wa kata, wahasibu na watendaji wa idara zingine.



Mkazi wa jijini Dar es Salaam akiwa na mzigo wa nyasi kwa ajili ya kulisha mifugo yake ikiwa ni kutekeleza sheria ya ufugaji wa majumbani eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kasi kinyonga, viwango duni ujenzi madarasa vyamkera Naibu Waziri

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amesema hajaridhishwa na kasi ya ujenzi wa madarasa katika mkoa wa Iringa. Kutokana na kutoridhishwa huko, ameutaka uongozi wa mkoa kuongeza kasi kuharakisha ukamilishwaji wa vyumba hivyo huku akisisitiza suala la ubora kuzingatiwa na thamani halisi ya fedha ionekane.

Silinde aliyasema hayo juzi baada ya kutembelea ujenzi wa vyumba vya madarasa katika halmshauri tano za mkoa huo, ambazo ni Kilolo, Manispaa ya Iringa, wilaya ya Iringa, Mufindi na Mji wa Mafinga.

Katika ukaguzi huo, alikuta halmashauri za Mufindi na Mafinga Mji ndizo zilizokamilisha ujenzi katika ubora wa hali ya juu kwa vyumba vyote zaidi ya 80 zilivyopewa na kukabidhi mkoani kwa ajili ya kupokea wanafunzi wapya.

Naibu Waziri alimwagiza Ofisa elimu wa Mkoa wa Iringa, Joyce Baravuga, kuongeza ufatiliaji katika sehemu zote ambazo bado ziko nyuma katika ujenzi kwa kuwa siku walizoongezewa zimebaki chache na ikiwezekana wafanye kazi usiku na mchana kukamilisha kazi hiyo.

Pia alisisitiza kuwa katika kufanya kazi hiyo wazingatie ubora kwa kuwa amegundua katika shule moja ya Kalenga ubora wake ni wa kiwango cha chini, hivyo wafanye vizuri zaidi ikiwezekana wakawaige Mufindi wamewezaje kufanya vizuri zaidi.

Mkuu wa Wilaya ya Mufundi, Saad Mtambule, alisema sababu kubwa ya kufanya vizuri katika ujenzi wa madarasa na kukamilisha kwa wakati na ubora unaotakiwa ni kufanya kazi kwa pamoja kama timu kutoka juu mpaka chini.

Alisema kwa kushirikiana kwa kila jambo wamechukua muda mfupi katika ujenzi ndani ya mwezi mmoja kwa kufanya kazi usiku na mchana na hata ilipobidi, gari la mkuu wa wilaya lilitumika kuhakikisha kazi inafanyika.

# Lukuvi ataja kiini migogoro ya ardhi

**Na Maulid Mmbaga**

WAKATI Mkoa wa Dar es Salaam ukitajwa kuwa kitovu cha migogoro ya ardhi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema migogoro ya aina hiyo inachangiwa kwa kiasi kikubwa na viongozi wa mitaa wakiwamo wenyeviti na maofisa watendaji.

Aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akimkabidhi Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makalla, mpango miji (master plan) ambao anaamini unakwenda kusaidia kumaliza migogoro ya ardhi iliyoshamiri katika mkoa huo.

"Wanaosababisha migogoro ya ardhi ni hao viongozi wa mitaa, mihuri yao inatumika vibaya sana. Mwenyekiti na watendaji wa mitaa wanafikia hatua kuchukua mpaka Sh. 700,000 kama vibali vya ujenzi na hazifiki kwa wakurugenzi, yaani wenyewe wamejianzishia serikali yao huko," alisema.

Lukuvi alisema viongozi hao wanafanya kila kitu mitaani kinyume cha sheria, akitolea mfano viongozi wa Halmashauri ya Kinondoni na watendaji wa Mabwepande ambako migogoro hiyo inatajwa kukithiri.

Alimtaka Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam (Makalla) kuunda kamati ya kushughulikia suala hilo.

"Vinginevyo watu wote tunaowamilikisha ardhi kwa heshima na kuwapa nyaraka na hati tukiamini kwamba hizo ndizo nyaraka salama kwa ajili ya ulinzi wa ardhi zao, itakuwa haina maana kama mtu anaweza kupata ardhi leo akapata na hati halafu mtu mwingine akaja na maneno akavamia, itaonekana kama sheria hazifanyi kazi," alisema.

Alibainisha kuwa wapo 'majambazi' wanaojulikana kama matapeli wa ardhi katika Mkoa wa Dar es Salaam, akisisitiza kuwa wanajulikana hadi kwa majina na kuna watu wana kampuni zaidi ya 70 ambazo zote zinahusishwa na utapeli wa ardhi.

Alisema baada ya kufanya uchunguzi, alibaini wapo wanaomiliki kwa anuani za Dar es Salaam lakini wanatoka nchi nyingine na hawajawahi kufika nchini na wanahusika kutapeli ardhi ya wananchi maskini.

Alisema Mkoa wa Dar es Salaam ndio kitovu cha hayo yote na aliahidi kushirikiana na mkuu wa mkoa huo kulishuhulikia hilo.

Lukuvi alisema wameandaa mpango miji wa mkoa huo kwa kuzingatia hatua zote, zikijumuisha kupiga picha ya anga ili kuona hali halisi ya eneo hilo ili wapangaji watekeleze upangaji wakiwa wanajua hali halisi ilivyo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Alibainisha kuwa watumiaji wakubwa wa mpango huo ni mamlaka za upangaji ambazo ni halmashauri za mkoa huo, ambao kila mmoja ataona mapendekezo yamependekeza mpango gani mapya wa matumizi ya ardhi.

"Nilikuwa naamini Dar es Salaam imejaa na wengi wanafikiri hakuna sehemu ya uwekezaji, nilitambua kwamba miji haijai kama unavyoona makaburi ya Kinondoni hayajai na miji nayo haijai, ila inapangwa inajizaa upya," alisema Lukuvi.

HABARI KITAIFA

# OSHA wazindua mpango mafunzo usalama kazini

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umezindua rasmi mpango wa mafunzo ya usalama na afya kwa taasisi za serikali na mashirika ya umma Tanzania Bara.

Mpango huo ambao umeanza kutekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa watumishi wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), umezinduliwa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu wenye Ulemavu), Ummy Nderiananga, aliyezitaka taasisi za serikali kujiandaa kuutekeleza.

"Ninatoa pongezi za dhati kwa menejimenti ya NIC kwa kutambua umuhimu wa mafunzo haya na kuamua kushirikiana na taasisi yetu ya OSHA katika kufanikisha jambo hili muhimu.

"Hivyo basi, niwasihi nyote mnaoshiriki mafunzo haya kuyazingatia na kwenda kuyatumia ipasavyo katika kuboresha utendaji wenu wa kila siku.

"Aidha, niwaagize OSHA kuhakikisha kwamba wanayafikia mashirika na taasisi zote za serikali na kutoa mafunzo ya usalama na afya kwa watumishi wote ambapo ni matumaini yetu kwamba endapo yatatolewa na kutekelezwa kikamilifu, basi yatasaidia kupunguza ajali, magonjwa na vifo vitokanavyo na mazingira ya kazi yasiyo rafiki.

"Hii itaisaidia serikali kuepuka gharama za kuwahudumia majeruhi wa ajali na wagonjwa pamoja na kuepuka hasara kubwa ambayo taifa limekuwa likipata kutokana na kupoteza nguvukazi yake na uharibifu wa mali na miundombinu," alisema.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mpango huo jana mkoani Morogoro, Mkurugenzi wa Usalama na Afya wa OSHA, Alexander Ngata, alitoa wito kwa taasisi za serikali kushirikiana na OSHA ili kufanikisha utekelezaji wa mpango huo ambao unahusisha ukaguzi wa usalama kwenye maeneo ya kazi pamoja na uchunguzi wa afya za wafanyakazi.

"Nitoe wito kwa waajiri katika sekta ya umma kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa mafunzo ya usalama na afya kwa watumishi wao, zoezi ambalo tutaliendesha sambamba na ukaguzi wa mifumo ya usalama na afya kwenye maeneo yao ya kazi pamoja na kuchunguza afya za wafanyakazi kama tulivyofanya kwa NIC," alisema.

Washiriki wa mafunzo hayo ambao ni viongozi wa NIC, waliipongeza OSHA kwa kuja na mpango huo waliouelezea kuwa ni mpango mzuri ambao mbali na kulinda afya na usalama wa wafanyakazi utaleta tija katika biashara na uzalishaji.

"Niwapongeze OSHA kwa kazi nzuri wanayofanya na niwaombe wajitahidi kuwafikia waajiri wengi zaidi kwani wakifanya hivyo hali ya usalama na afya itazidi kuimarika nchini jambo ambalo litatusaidia kuimarisha mifuko ya bima kutokana na kupungua kwa gharama za fidia za majanga mbalimbali," alisema Lihami Masoli, Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa NIC.

Masoli alishiriki mafunzo ya Huduma ya Kwanza yaliyotolewa na OSHA kwa menejimenti ya shirika pamoja na watumishi wengine.

Miongoni mwa majukumu ya OSHA ni kukuza uelewa wa masuala ya usalama na afya miongoni wa Watanzania kupitia kutoa mafunzo mbalimbali ikiwamo mafunzo ya huduma ya kwanza mahali pa kazi.

Pia mafunzo kwa wanakamati za usalama na afya mahali pa kazi, uchunguzi wa ajali mahali pa kazi, tathmini ya vihatarisha vya usalama na afya mahali pa kazi pamoja na kozi nyinginezo zinazohusu masuala ya usalama na afya mahali pa kazi.

# Jela miaka 10 kujaribu kumuua mkewe

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza, iliyoketi mjini hapa, imemhukumu Peter James (56) kutumikia kifungo cha miaka 10 jela kwa kosa la kujaribu kumuua mke wake.

James alifanya jaribio la kumuua mke wake, Nyabahimba Msubi, kwa kumcharanga mapanga shingoni na mkononi, hivyo kumsababishia maumivu makali sehemu za mwili wake kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji wa Mahakama hiyo, Mwanabaraka Mnyukwa, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hili pasipo kuacha shaka yoyote.

Jaji Mnyukwa alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia ya kikatili kama yake.

Alisema upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Lusiana Shabani, ulipeleka mashahidi watatu pamoja na vielelezo viwili ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa alijaribu kumuua mke wake.

Upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili wa Kujitegemea Erick Lutehanga, haukuwa na shahidi wala kielelezo bali mshtakiwa alijitetea peke yake.

Jaji Mnyukwa alisema siku ya tukio mlalamikaji alikuwa akipika nyumbani kwake majira ya saa 3:00 na alimwona mshtakiwa umbali wa mita 17 na alipofika mita tatu alimsalimia na mlalamikaji hakuitika na kuanza kukimbia ndipo mshtakiwa alimkata panga kwenye mkono wa kulia.

"Nimeangalia ushahindi wa pande zote nimegundua kuwa upande wa Jamhuri umethibitisha kosa pasipo kuacha shaka yoyote, hivyo mahakama inakutia hatiani mshtakiwa kwa kosa la kujaribu kumuua mke wake. Pia mahakama inamtaka mshtakiwa ajitetee ili mahakama impunguzie adhabu.

Mshtakiwa akiongozwa na Wakili Lutehanga, aliomba mahakama imwonee huruma mteja wake kwa sababu ana watoto sita ambao wanamtegemea.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili Lusiana Shabani, uliomba mahakama hiyo itoe adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na jamii nzima ili kupunguza ukatili uliopo mkoani Geita.

Jaji Mnyukwa alitupilia mbali utetezi huo na kusema: "Mshtakiwa nakuhukumu kwenda jela miaka 10 ili ukajifunze namna ya kuishi na jamii. Ukimaliza kifungo chako utakuwa raia mwema na rufani iko wazi kwa upande ambao haujaridhika na uamuzi huo.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga Adam Malima akiongea na washiriki kabla ya kufungua kikao kazi cha Tathmini ya Afya ya Msingi na Uzinduzi wa Mradi wa kuongeza muitikio wa kuchanja chanjo ya Uviko 19 Mkoa wa Tanga jana ambacho kilishirikisha Wizara ya Afya, TAMISEMI, Shirika la Amref na wataalamu wote wa afya wa mkoa. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# Serikali yatambua mchango mashirika uhifadhi mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amesema serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGO) katika shughuli za uhifadhi wa mazingira.

Dk. Jafo alitoa kauli hiyo jana alipofungua kongamano la kukomboa ardhi iliyochakaa katika nyanda kame za Tanzania na maadhimisho ya miaka 10 ya Shirika la Lead Foundation.

Alisema kongamano hilo linatoa taswira ya namna gani NGO zinashiriki kikamilifu katika kusukuma mbele ajenda ya mazingira nchini, hivyo kuwajenga uelewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira.

"Niliwahi kuitisha mkutano na mashirika yanayojihusisha na suala zima la mazingira na leo (jana) ninajisikia faraja kubwa kuona mashirika haya yanapiga hatua na lengo langu kubwa ni kuona kila mmoja anashiriki katika suala zima la uhifadhi wa mazingira," alisema.

Waziri Jafo alisema serikali itaendelea kusimamia kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira inayowashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wadau kutoka mashirika hayo. Alisema anafarijika kutokana na Mpango Mkakati wa Miaka 10 uliozinduliwa na Lead Foundation ambao unaonyesha namna linavyoiunga mkono serikali katika kutunza na kuhifadhi mazingira hususan katika eneo la mabadiliko ya tabianchi linaloikabili dunia.

Alitumia nafasi hiyo kutoa rai kwa wanachi kutumia kipindi hiki cha masika kupanda miti kwa wingi na kuitunza ili kukabiliana na ukame ambao huleta athari mbalimbali za kijamii.

Aliwaelekeza wakuu wa mikoa na wilaya kusimamia vizuri upandaji miti na kuhakikisha misitu haichomwi ovyo ili kuepusha athari za mabadiliko ya tabianchi zinazochangia kukosekana kwa mvua.

Mwanzilishi wa Shirika la Lead Foundation, Askofu Dk. Simon Chiwanga, alisema kazi ya ukombozi wa mazingira inafanywa kwa namna mbili ambazo ni kuelimisha na kumbadilisha mtu fikra.

"Ninafurahia sana uwapo wako hapa mheshimiwa waziri na hiyo ari, hiyo huruma na upendo ulio nao tunamwomba Mungu akubariki sana," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vipaji Samia Taifa Cup muhimu kuendelezwa

**KWA** mara nyingine wadau wa michezo Tanzania wameshuhudia mashindano ya ngazi ya kitaifa yaliyojulikana kwa jina la Samia Taifa Cup 2021, ambayo yamemalizika hapa jijini Dar es Salaam juzi.

Mashindano hayo ya Samia Taifa Cup yalishirikisha mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani na yalikuwa katika michezo mitatu.

Michezo hiyo ni riadha (wanaume na wanawake), netiboli (wanawake) na soka ambalo lilishirikisha timu za wanaume na wanawake.

Katika mchezo wa netiboli, mabingwa wa michuano hiyo iliyoanza mapema mwezi huu ni Mjini Magharibi na mkoa huo ukichukua tena ubingwa wa soka kwa wanaume na riadha huku soka la wanawake vinara ni jiji la Arusha.

Lengo kuu la kufanyika kwa mashindano hayo ni kuwapa nafasi wachezaji kutoka mikoa yote ya Tanzania kuonyesha vipaji vyao baada ya kukosa kusajiliwa na timu zinazoshiriki ligi mbalimbali hapa nchini.

Na kupitia michuano hiyo, tunaamini makocha wa klabu na timu za taifa za michezo hiyo mitatu iliyoshindaniwa watakuwa wamepata nyota wapya kwa ajili ya kuboresha vikosi vyao kuelekea msimu mpya wa mashindano.

Lakini wakati mikoa inafurahia kurejea nyumbani na makombe na medali za ushindi, ni vyema wasimamizi wakaendelea kuwatunza wachezaji wao ili vipaji walivyonavyo vikaendelea kuimarika na baadaye wakalisaidia taifa pale watakapoitwa katika vikosi vya nchi.

Kuwaacha wachezaji hawa mpaka mashindano mengine hapo mwakani, haitakuwa jambo sahihi kwa sababu nguvu zilizotumika kuwaandaa zitapotea na nchi itarejea kule kule kuwa washiriki badala ya washindani, pale timu zake zitakapokwenda kushindana kimataifa.

Tunawakumbusha viongozi wa mikoa ambayo haikushiriki michuano hii, kuanza maandalizi mapema kwa ajili ya michuano ya mwakani kwa sababu kuendelea 'kukacha' kushiriki, sio tu kunawanyima wachezaji nafasi ya kuonekana, lakini mnachangia kurudisha nyuma maendeleo ya mkoa husika.

Ni sifa pale mkoa utakapobaini mchezaji au wachezaji wake wamesajiliwa na timu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Kuu ya Wanawake, Ligi ya Championiship baada ya kuonekana wameng'ara kupitia michuano hii ya Samia Taifa Cup.

Tukumbuke miaka ambayo Tanzania ilikuwa inafanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa ya mpira wa miguu, netiboli na Michezo ya Olimpiki, washiriki wengi walitokana na michuano kama hii na kilichofuata ni kuwaendeleza wachezaji hao na baadaye waliiletea nchi heshima kwa kurudi na medali.

Katika kuthibitisha serikali imedhamiria kuleta mapinduzi kwenye tasnia zote, pia wasanii mbalimbali walichuana kuwania tuzo zilizoandaliwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.


Wasanii waliofanya vizuri walitambuliwa, lakini ili nyota hawa wapya waendelee kuitendea haki sanaa wanayoifanya, wanatakiwa kupewa mafunzo na hatimaye huko mbele wanaweza kuja kuwa wasanii tishio na watakaofanya vizuri ndani na kwenye soko la kimataifa.

Ili timu, wachezaji au msanii afanye vizuri katika mashindano yoyote atakayoshiriki kuanzia ngazi ya kata, wilaya, mkoa, taifa na kimataifa, basi hakuna njia ya mkato zaidi ya kuwapo kwa maandalizi bora na kwa kutumia makocha wenye sifa na taaluma ya kila mchezo.

Tunaikumbusha mikoa, kumalizika kwa mashindano ya mwaka huu, ndio mwanzo wa maandalizi ya michuano ijayo ambayo tunatarajia kuona ushindani umeongezeka maradufu kwa malengo ya kuinua sekta ya michezo hapa nchini.

Mafanikio katika michezo kamwe hayapatikani kwa miujiza, mafanikio yote huja baada ya kuwapo kwa maandalizi sahihi na si ya kukurupuka zikiwa zimebakia siku chache kabla ya kuanza kwa michuano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Safi Jeshi la Polisi kukamata jezi feki

Na Adam Fungamwango

**JUZI** Jeshi la Polisi lilitangaza kuwakamata wafanyabiashara 11 na kuwafungulia mashtaka kuhusiana na tuhuma za utengenezaji na uuzaji wa jezi feki. Msemaji wa jeshi hilo, David Misime, alisema hayo jijini Dodoma, ambapo amedai ukamatwaji huo umetokana na msaada kutoka kwenye viwanda vinavyotengeneza jezi halisi.

Mbali na hilo, jeshi hilo likasema limekamata jezi feki za klabu ya Simba 279 na watuhumiwa 15 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza ambao walikutwa na jezi hizo wakiziuza.

Msemaji huyo akaongeza kuwa kitendo hicho ni kuinyima au kuidhulumu serikali mapato kutokana na ukwepaji wa kodi.

"Kama inavyofahamika baadhi ya timu huingia mikataba na makampuni kwa ajili ya utengenezaji wa jezi na makubaliano rasmi na jezi zinapouzwa kwa kiasi fulani cha pesa hupatiwa kwa ajili ya kulipa mishahara ya wachezaji na huduma nyingine, nawataka wananchi kuendelea kutoa taarifa wanapoona jezi feki zinauzwa ili kukomesha tabia hiyo," alisema Misime.

Hii ni taarifa nzuri mno kwa wadau wote wa soka nchini Tanzania. Ni kilio cha muda mrefu sana. Klabu zimekuwa zikinyonywa miaka nenda rudi kwa watu kuuza jezi feki na kujipatia fedha haramu.

Klabu za Tanzania zimekuwa masikini miaka nenda rudi zikishindwa hata kulipa mishahara wachezaji.

Ukiziangalia Simba na Yanga ambazo zimeanzishwa miaka ya 80 zimeshindwa kujiendesha zenyewe kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo wizi kama huu.

Ukizingalia klabu hizi zina mashabiki kila kona ya nchi. Siku zikicheza mechi na timu nyingine au zenyewe kwa zenyewe mamia ya mashabiki wanakuwa wametinga jezi za timu hizo. Tatizo sasa ni kujua feki zipi na halisi ni zipi.

Hata baadhi ya viongozi wa klabu hizi wanadaiwa kushiriki kwenye biashara hizo haramu. Na hasa wale wa zamani kabla ya klabu hizi kuingia kwenye mfumo wa mabadiliko. Na siku zote viongozi hao wamekuwa ndiyo kikwazo kwa wauza jezi feki kukamatwa. Siyo kwamba walikuwa wanawakingia kifua, lakini walikuwa hawatoi ushirikiano kwa vyombo vya usalama kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mabadiliko ya Uendeshaji wa klabu ya Simba, pamoja na udhamini wa Yanga ambapo wadhamini wake ndiyo wanaotoa, kusambaza na kuuza jezi, umeanza kuleta matunda kwa sababu wao wameanza kudhibiti jezi feki.

Hawa ndiyo wanaotaka mabadiliko ya kweli kwenye soka la Tanzania kwa sababu wanatoa pesa nyingi kuziendesha klabu hizi, hivyo wanataka kudhibiti mapato.

Nalipongeza Jeshi la Polisi kwa kuanza kufanya kazi hii ambayo ilionekana kama vile imeshindikana miaka ya nyuma kutokana na kukosa ushirikiano. Kutokana na kupata ushirikiano kutoka kwa baadhi ya viongozi, ilionekana kama vile jeshi linasuasua na kulaumiwa na baadhi ya wachambuzi wa soka , lakini sasa inaonekana si hivyo.

Walichokuwa wanataka Polisi ni ushirikiano kutoka kwa klabu na watengeneza jezi halisi, ili waifanye kazi yao kwa ufanisi kama ambavyo kwa sasa tunaona.

Kitakachotokea kwa sasa ni wahujumu wataogopa kutengeneza na kuuza jezi feki. Sio kwamba hili suala litaisha kabisa, kwa sababu uhalifu wa aina hii upo hata Ulaya kwenye klabu kubwa na vyombo vya kisasa vya usalama, lakini bado jezi feki zipo.

Ila kutakuwa na woga kidogo kwa wanaofanya shughuli hiyo, na pia hata wakikamatwa watakuwa wakipelekwa mahakamani, tofauti na zamani ambapo walikuwa huru kwa asilimia 100.

Kitakachotokea ni jezi zitakazokuwa zinaenea asilimia kubwa zitakuwa halisi, na hii haitazisaidia timu kubwa za Simba na Yanga, bali hata zisizokuwa na mashabiki wengi kama vile Azam FC, Mbeya City na Geita Gold.

Kwa moto huu wa Jeshi la Polisi ambao imeanza nao, mbele ya safari klabu zinaweza kuanza kujiendesha kwa fedha za jezi, lakini pia hata kusajili wachezaji wa gharama kubwa kutokana na mauzo.

Tumeshuhudia umati mkubwa wa mashabiki wa klabu za Simba na Yanga zikifurika kwenye maduka ya kuuza jezi za msimu unapoanza. Kwa umati ule kama wote watakuwa wakinunua jezi halisi, haina mashaka klabu hizi hazitokuwa masikini tena.

Makampuni yaliyopata tenda yatapata faida na klabu pia zitapata fedha zitakazosaidia kuendesha baadhi ya mambo muhimu ya kiutawala.

Huu uwe ni mwanzo tu kwa Jeshi la Polisi, lakini pia wanahitaji msaada na ushirikiano kutoka kwa wananchi wenyewe, wasamaria wema, wanachama na mashabiki wa klabu, viongozi pamoja na makampuni.

## HABARI KITAIFA

# Wanahabari waambiwa upotoshaji ni dhambi

**Na Christina Haule,** DODOMA

WANAHABARI wametakiwa kuepuka dhambi ya upotoshaji ambayo ni sawa na dhambi ya kuua mtu bali waitumie taaluma yao katika kazi ya kuelimisha jamii juu ya kujikinga na janga la ugonjwa wa virusi vya Corona, kama inavyotakiwa kitaalamu.

Mtaalamu wa Afya kutoka Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, Idara ya Kinga Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. William Shayo, alisema hayo jana wakati akizungumza na wanahabari juu ya imani na taarifa potofu juu ya chanjo ya corona.

Dk. Shayo alisema imani na taarifa potofu hazina uthibitisho wenye mashiko huku zikiwa zina sifa mbaya za uzushi ambazo jamii huzibeba kwa haraka.

"Ikumbukwe kuwa ukifanya mtu mmoja asipate chanjo au tiba unaweza kusababisha mtu huyo kufariki dunia na kifo chake kinaweza kuleta shida kwa wengine ikiwamo familia yake," alisema.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wanahabari kuacha kuripoti taarifa potofu juu ya corona kwa kuwa imani na taarifa potofu husambaa kwa kasi sana na kusababisha wengine kutochanja na kutishia uhai wao.

Alitaja baadhi ya maneno ya uzushi na upotoshaji kuwa ni chanjo zinafanya mtu anakuwa kwenye kundi la kufuatiliwa jambo ambalo si kweli kwa sababu kama wangetaka kuweka ufuatiliaji wangeweka kwenye chanjo mbalimbali za awali.

Dk. Shayo alitaja kauli nyingine kuwa ni chanjo kuathiri via vya uzazi na nguvu za kiume jambo ambalo pia si kweli kwa sababu akiwa mmoja wa waliochanja tayari mke wake ni mjamzito.

Aliwataka wanahabari kuhakikisha jamii inapata chanjo kwa asilimia 95 hadi Desemba, mwakani baada ya kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuchanja wakiwamo walioko vijijini ambao hawakufikiwa mwanzoni kwa kutumia taarifa za kitafiti zilizopo.

Alisema hali ya homa kwa mtu aliyepata chanjo ni kawaida sababu hata watoto huwa wanapata homa na homa si ugonjwa bali ni hali ya kinga za mwili kupambana na ugonjwa.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alipongeza serikali kwa kuamua kuzitumia Sh. trilioni 1.3 zilizotolewa kwa ajili ya mapambano dhidi ya corona katika kuimarisha miundombinu ya maji na elimu ili kuboresha maana ya jamii kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema ujenzi wa madarasa unaoendelea utasaidia wanafunzi kukaa mbalimbali madarasani sambamba na uchimbaji visima kwa kuwapo na mpango wa kupeleka gari la kuchimba kisima kila mkoa na kuacha kutegemea gari moja lililopo nchini kwa sasa ili kuhakikisha kila eneo linakuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji ya kujiepusha na virusi vya corona.

Hata hivyo, alisisitiza wanahabari kuona haja ya kuelimisha jamii na watoto kwa ujumla na kuwafanya kujitambua kujikita kwenye elimu sambamba na kutafuta ajira binafsi ili waweze kujikimu katika maisha.

# Mbarawa aibua madudu ujenzi jengo la abiria uwanja wa ndege

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amegundua kasoro katika ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza, hivyo kumwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), kupeleka mara moja mhandisi kwenye mradi huo.

Amesema jengo hilo linalojengwa kwa gharama ya takribani Sh. bilioni 11, halijakidhi viwango vya kimataifa na kuna makosa mengine yanayohitaji wataalamu zaidi kushauri namna gani ifanyike ili kukidhi viwango.

Prof. Mbarawa alisema hayo juzi jijini Mwanza alipofika kukagua ujenzi wa jengo hilo unaoendelea ambao mpaka sasa umefikia asilimia 85 na kutoridhishwa na hali halisi, hivyo kubainisha kuwa umekosa vigezo vya kimataifa vinavyosimamiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO).

"Mwenye dhamana ya viwanja vya ndege si mkoa wala halmashauri bali ni TAA. Nashangaa kusikia hakuna mhandisi anayesimamia jengo hili kutoka kwao. Naagiza watoke Dar es Salaam waje kusimamia hili jengo ili tupate thamani ya fedha na viwango vinavyostahili. Hatutaki kufanya makosa halafu baadaye tuje tulaumiane," alisema Prof. Mbarawa.

Ameongeza kuwa majengo yanayostahili kujengwa katika viwanja vya ndege vya kimataifa ni tofauti na majengo mengine kwa kuwa yana viwango vinavyostahili ambavyo katika uwanja huo havikufuatwa.

"Tunatakiwa kujenga jengo litakalodumu miaka 20 hadi 30. Hatuwezi kujenga hivi hivi tu hapa tulipofikia, wataalamu waje waangalie nini kiboreshwe ili jengo likidhi mahitaji", alisisitiza.


Prof. Mbarawa alisema serikali inaendelea kuboresha viwanja vingi vya ndege nchini na kwamba cha Mwanza kinatarajiwa kuwa cha kimataifa, hivyo lazima fedha zinazotolewa thamani yake ionekane na kupitishwa kwa viwango vya ICAO.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alisema mkoa umeshaunda timu ya wataalamu na tayari wametoa michoro sahihi na kazi zinaendelea za kuboresha jengo hilo ili likidhi viwango vinavyostahili.

Katibu Tawala Msaidizi wa Miundombinu, Chagu Nghoma, alimweleza Waziri kuwa jengo hilo la abiria litakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria laki nne kwa mwaka.

Pia alisema jengo litakuwa na ukumbi wa abiria wa ndani, wa kimataifa, ukumbi wa abiria mashuhuri, migahawa na maduka, ofisi mbalimbali za serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Uhamiaji, Afya, Polisi na Maliasili na pia litakuwa na eneo la kuegesha magari takribani 320.

Ujenzi wa jengo hilo ulianza Septemba 19, mwaka huu na unatarajiwa kukamilika mwaka ujao.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akipata maelezo kutoka kwa Msimamizi wa Kituo cha Kusambaza Umeme cha Mbagala, Mhandisi Neema Ngogo, wakati wa ziara ya kutembelea kituo hicho jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Fedha za corona zajenga madarasa 247

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WILAYA ya Kahama mkoani Shinyanga imekamilisha ujenzi wa vyumba 247 vya madarasa katika shule za msingi na sekondari kupitia Sh. bilioni 5.6 za corona zilizotolewa na serikari.

Fedha hizo zilitolewa miezi miwili iliyopita na kujengwa kwa vyumba vya madarasa katika halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama ili kuwezesha wanafunzi waliochaguliwa kuanza masomo mwakani wanaingia madarasani wote.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Festo Kiswaga, alisema hayo jana wakati akikabidhiwa vyumba hivyo na wakurugenzi wa halmashauri hizo.

Alisema kwa sasa vyumba hivyo vinasubiri wanafunzi waliochaguliwa kuanza masomo mwakani, hivyo jukumu lililobaki ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaingia madarasani.

Kiswaga alisema wilaya ilipokea Sh. bilioni 5.6 za ujenzi wa vyumbva vya madarasa 247 huku halmashauri ya Msalala ikipata Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa 90, Ushetu Sh. bilioni 1.6 kujenga vyumba 60.

Alisema Manispaa ya Kahama ilipata Sh. bilioni 2.2 kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa 97 na bweni moja kwenye shule yenye mahitaji maalumu na kwamba vyote vimekamilika katika muda uliopangwa.

"Madarasa yamekamilika katika halmashauri zote na yana madawati, viti na meza na sasa yanasubiria wanafunzi waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwakani. Nguvu hii tuliyoitumia katika ujenzi huu tuitumie kuhakikisha wanafunzi wote wanaingia madarasani," alisisitiza.

Kiswaga aliweka bayana kwamba fedha hizo zilimtia hofu kubwa baada ya kuzipokea na kwamba kumalizika kwa ujenzi wa vyumba hivyo kumemtoa hofu na sasa yuko huru na anajiandaa kumkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, hivi karibuni.

Makamu Mwenyekiti wa Manispaa ya Kahama, Sindano Wiliam, ambaye ni Diwani wa Nyihongo, alisema kulipojengwa sekondari mpya alisema kukamilika kwa madarasa hayo kutawapunguzia adha wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda shule za kata jirani kama ilivyokuwa awali.

Akizungumza kwa niaba ya wakurugenzi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Mwalimu Lino Mwageni, alisema wamemaliza ujenzi wa madarasa kwa kiwango walichopangiwa na serikali.

# Tahadhari maambukizi mapya VVU utekelezaji mradi Benki ya Dunia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wilayani Kahama wametakiwa kuwa makini wakati wa utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa Miundombinu katika miji Tanzania (TACTIC) utapoanza ili kuepukana na maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mtaalamu Mshauri wa Mazingira kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Kayonko Juma, katika kikao kilichohusu mpango wa uboreshaji wa miundombinu katika miji Tanzania kupitia mpango wa Benki ya Dunia. Manispaa ya Kahama ni moja ya maeneo ya utekelezaji wa mradi huo. Alisema kutokana na mji wa Kahama kukua kwa kasi na kuwa na ongezeko kubwa la watu, mradi huo unaweza kuwa chanzo kikubwa cha maambukizi ya VVU kwa kuwa wafanyakazi watakaokuwa wakitekeleza mradi huo watakuwa ni wengi na watatoka katika maeneo mbalimbali.

Juma pia alisema katika miradi mikubwa ambayo imekuwa ikitekelezwa na serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, kumekuwapo na matatizo mengi na ili kuyadhibiti, serikali imejipanga vizuri kwa lolote litakalojitokeza.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema ili kuhakikisha kutokuwapo kwa maambukizi mapya ya VVU wakati wa utekelezaji wa mradi, watawapatia elimu wananchi juu ya magonjwa ya kuambikizwa na na yasiyoambukizwa ili wananchi wawe katika hali ya usalama kipindi chote cha mradi. Pia alisema wananchi wa Kahama wamekuwa na kero kubwa ya mitaro kwa kuwa mvua zinaponyesha, maji yote yamekuwa yakijaa katika maeneo ya barabara na kuwataka wananchi na wadau wote kutoa ushirikiano ili kuwezesha ujenzi huo kukamilika kwa asilimia 100 na kwa muda uliopangwa.

Akitoa ufafanuzi kuhusu mradi huo, Mhandishi kutoka TAMISEMI kitengo cha miradi inayotekelezwa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Rashid Mtamila, alisema miradi hiyo imekuwa na matatizo mengi ikiwemo ukuaji wa miji na ongezeko la watu.

Changamoto nyingine, alisema ni pamoja na miji mingi kutojiandaa kukabiliana na ongezeko la watu huku baadhi ya halmashauri zikiwa hazina miundombinu ya kukabiliana na majanga yanayoweza kutokea kipindi chote cha utekelezaji wa mradi.

Alisema katika halmashauri 45 zinazotarajiwa kunufaika na mradi huo, Kahama imekuwa katika kundi la kwanza kutokana na mji huo kukua kwa kasi pamoja na ongezeko kubwa la watu.




Kaimu Meneja wa Benki ya NMB kanda ya mashariki, Harold Lambileki akimkabidhi mshindi wa kampeni ya Bonge la Mpango wa pikipiki ya mizigo ya matairi matatu, Sadick Ali Said kutoka tawi la NMB Ifakara. Tayari Benki ya NMB imeshatoa zawadi ya pesa taslimu Milioni Kumi na pikipiki 26 katika kampeni hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu watakiwa kuzingatia maadili

**Na Christina Mwakangale**

WAHITIMU wa kada ya afya wametakiwa kufanya kazi kwa weledi, kuzingatia kanuni na maadili ya taaluma, kila mara wanapotoa huduma kwenye jamii.

Hayo yalibainishwa juzi mkoani Dar es Salaam na mgeni rasmi, Prof, Eliab Opiyo, kwenye mahafali ya kwanza ngazi ya stashahada ya wafamasia katika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha St. Maria.

Prof. Opiyo ambaye pia ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha St. Joseph, alisema ndani ya jamii kuna uhaba wa wahudumu wa afya kwenye hospitali za umma na binafsi, hivyo mafunzo waliyoyapata yawe na tija sambamba na kufuata miongozo ya taaluma.

"Wafamasia huwa wanahitajika zaidi nchini kwa kuwa kuna uhaba. Hospitali za umma, binafsi kuna mahitaji. Vyuo binafsi tutaendelea kutoa mafunzo ya kada hii ili kukabiliana na uhaba wa wataalamu hao" alisema Prof Opiyo.

Mkurugenzi Mtendaji St. Maria, Dk Thompson Ananth, alisema wahitimu hao wasisubiri kuajiriwa, badala yake waandae maandiko yenye wazo la ubunifu wa biashara inayoendana na taaluma yao na kisha kutoa ajira.

"Kuna fursa nyingi katika sekta hii, mnatakiwa kuandika wasilisho la biashara kulingana na taaluma yenu. Mlichojifunza mkakitumie kwenye jamii, mkawe mabalozi wazuri wa chuo kinidhamu," alisema Dk. Ananth.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo, Dk Otilia Gowelle, alisema wahitimu 53 wamehitimu kozi ya ufamasia, idadi ambayo ni ndogo, hivyo akasisitiza kuwa kuna haja ya kuongeza wataalamu wa afya ili huduma kuboreka.

# Wapaza sauti kero upatikanaji maji Masasi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAKAZI wa kijiji cha Mlingura, Masasi mkoani Mtwara, wanakabiliwa na uhaba wa maji safi na salama, hivyo kulazimika kununua ndoo ya lita 20 kwa Sh., 1,000.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hii jana kijijini hapo, wakazi hao walisema hali ya upatikanaji wa maji safi na salama katika kipindi ambacho mvua hazijaanza kunyesha ni ngumu na inaathiri shughuli zao za kiuchumi.

Muhaji Awadh, mkazi wa kijiji hicho alisema inapofika kiangazi, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo yao ni shida, hivyo wananchi wanalazimika kuacha shughuli za maendeleo na kutumia muda mwingi kusaka maji.

Alisema kwa miaka mingi sasa kumekuwa na idadi kubwa ya viongozi wanaofika katika kijiji hicho na kutoa ahadi ya kupeleka maji ya bomba pamoja na kuchimba visima virefu lakini hadi sasa hazijatekelezwa.

Kwa mujibu wa Awadh, kutokana na hali hiyo, wanaiomba serikali kuwasaidia kuwapelekea huduma hiyo ili waondokane na adha hiyo ambayo imekuwa ikikwamisha upakanaji wa maendeleo kwenye kijiji chao kwa vile badala ya kufanya kazi za maendeleo wanatumia muda huo kusaka maji.

Naye Fatuma Dustan, alisema kutokana na kero hiyo, baadhi ya wanawake wameamua kusitisha huduma ya uzazi kwa sababu hata kama watajifungua watoto, hakuna maji ya kuwafanyia usafi, hivyo wanasubiri hadi pale serikali itakapowapelekea maji.

"Kwa mfano mimi kama mwanamke kwa sasa nimeamua kusitisha huduma ya kuzaa au kupata ujauzito kwa sababu naona kijiji chetu hakina huduma ya maji. Hata kama ukisema uzae watoto wataoga nini wakati maji ni shida?" alihoji.

Mwenyekiti wa Kijiji, Leonce Hamisi, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo jambo ambalo alisema kwa sasa wananchi wananunua maji kutoka kwa watu ambao wanapitisha na kwamba ndoo moja ya lita 20 inauzwa kati ya Sh. 800 na 1,000.

Alisema kazi za kiuchumi kwa sasa hazifanyiki kwa sababu wananchi wanatembea umbali mrefu kwenda vijiji vya mbali kwa ajili ya kutafuta maji. Alisema kutokana na adha hiyo. wanaiomba serikali kufanikisha suala la upatikanaji maji haraka.

Dominick Milanzi, Diwani wa Mlingura, alisema kero ya maji katika kijiji hicho imekuwa sugu kwa kuwa licha ya kuisemea mara kwa mara katika vikao vya baraza la madiwani, imekuwa shida kupatiwa ufumbuzi.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Masasi, Juma Yahaya, alisema upatikanaji wa huduma ya maji kwa wilaya ya Masasi ni wa kuridhisha japokuwa katika kipindi cha hivi karibuni imepitia katika wakati mgumu kwa sababu ya kiangazi kwa sababu ya maji kukauka visimani.





# Watakiwa kushiriki sensa watu, makazi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATANZANIA wameshauriwa kujitokeza kwa wingi kushiriki sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 2022 kwa maendeleo ya taifa na kuacha kusikiliza maneno ya uzushi katika mitandao ya kijamii.

Rai hiyo ilitolewa jana na Makamu Askofu Mkuu wa Kanisa la Cornerstone Pentecost Tanzania, Yohana Mgusi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema Watanzania wanatakiwa kujitokeza kwa wingi katika sensa hiyo ambayo ni tukio la kiserikali la kuhesabiwa ambalo litawezesha kupanga bajeti kwa ajili ya maendeleo ya kila Mtanzania.

Alisema badala ya kujengewa hofu kama ilivyo kwa ugonjwa wa corona, Watanzania wajitokeze kuiunga mkono serikali kwenye jambo hilo muhimu ambalo linalenga kumfikia kila Mtanzania bila kujali itikadi ya kidini na kisiasa.

"Ninawaomba Watanzania wezangu tujitokeze kwenye zoezi hili muhimu litakalofanyika mwakani kwa kila mtanzania ahesabiwe ili serikali yetu iweze kupanga bajeti yake kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu"alisema

Askofu Mgusi pia aliwaomba Watanzania kuondoa vikwanzo katika utoaji wa majibu kwa watumishi watakaokuwa na jukumu la kuhesabu wakati huo.

Alisema badala yake watoe ushirikiano utakaowezesha zoezi hilo kwenda kwa wakati na wepesi pale watakapotoa majibu yaliyo sahihi yenye tija kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Pia aliziomba familia ambazo zinaishi na watu wenye ulemavu kutowaficha kwenye zoezi hilo kwa kuwa wao pia wana haki ya kuhesabiwa kama ilivyo
kwa wengine bila kujali hali zao.

Kitendo cha kuwaficha ni dhambi tena ni cha ukatili na unanyanyasaji na watakaobainika serikali isiwafumbie macho bali iwachukulie hatua za kisheria ili kukomesha tabia hiyo.

Askofu huyo awali aliwataka wazazi na walezi wenye watoto wanaotakiwa kwenda shule kutowaweka majumbani.

# Askofu ahimiza waumini kufanya kazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dickson Chilongani, amewataka waumini wa kanisa hilo kujishughulisha na ujasiriamali na vikundi vya vikoba ili kuondokana na umaskini.

Dk. Chilongania alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akifunga mafunzo ya vikoba na ujasiriamali kwa wanawake wa Ushirika wa Mama wa Kikristo wa Kanisa Anglikana Tanzania (UMAKI)

Alisema mafunzo ya ujasiriamali ni muhimu kwa wakati huu kwa waumini wa kanisa hilo nchini ili kuondokana na umaskini katika kaya zao.

"Kuna watu wanaishi kana kwamba Yesu anarudi kesho. Mtu ana maisha magumu lakini hana shamba wala hajishughulishi na ujasiriamali watoto wanapata shida hata kwenda shule ni shida.

"Tunapaswa kubadilika, walipokuja wamisionari kuleta dini walitufanya kuona kuwa mtu ukishaokoka basi wewe huna sababu ya kushughulika na ujasiriamali au uzalishaji mali lakini wao walipokuja walifanya kazi na walichuma mali hapa hapa kwetu na kwenda nazo kwao na sisi tukaendelea kuwategemea wao," alisema.

Dk. Chilongani alisema kinachotakiwa hivi sasa si waumini kupatiwa msaada wa fedha bali ni kuwezeshwa ili kubadili mitizamo yao.

"Hata Yesu mwenyewe anatusisitiza kufanya ujasiriamali. Walikuja wamisionari waliotuaminisha kuwa hatuna sababu ya kufanya kazi lakini tulipoisoma Biblia wenyewe tumebaini kuwa kufanya kazi ni jambo la lazima. Tusiwe kama yule aliyepewa talanta moja akaichimbia chini bali tuzalishe zaidi kwa kile tulicho nacho," alisema.

Pia alisema Watanzania wanaweza kutumia fursa pamoja na rasilimali zilizopo nchini ili kujikwamua kiuchumi badala ya kuendelea kutegemea misaada.

"Tukifanikiwa kuimarisha maisha ya waumini wetu hata kanisa linatakuwa imara lakini kama maisha ya waumini wetu yataendelea kuwa duni, basi hata huduma ya kanisa itakuwa duni.

"Hatujui Yesu atarudi lini lakini inashangaza watu wanaoishi kama Yesu anarudi kesho. Hawafanyi kazi wala hawana shughuli yoyote ile ya kujipatia kipato. Lazima tubadilishe mitizamo yetu na viongozi wa dini tusione aibu kufundisha hivyo kwani ipo kwenye Biblia," alisisitiza.

Aliongeza kuwa kwa wakati huu semina za ujasiriamali na vikundi vya vikoba kwa waumini ni muhimu kwa sababu kanisa bila fedha haliwezi kuendelea.

Kadhalika aliagiza viongozi wa mitaa yote zilizoko chini ya dayosisi hiyo, kuhakikisha wanawekeza miradi mbalimbali ambayo wataitumia kama vitega uchumi.

"Lazima kila Parish (mtaa) kuwa na mradi hata mmoja kila eneo nataka kuwa na mradi kama fremu za maduka au nini lakini kuwapo na mradi wa kitega uchumi cha kanisa," alisema.

Mratibu wa UMAKI Kanisa Anglikana Tanzania, Magreth Ndonde, alisema mafunzo hayo yametolewa kwa siku tano yakijumuisha zaidi ya washiriki 40.



Baadhi ya washiriki wa mkutano mkuu wa mwaka wa afya mazingira na usafi uliofanyika jana Jijini Dodoma kwa kuwashirikisha wawakilishi kutoka Mikoa ya Tanzania pamoja na wadau wengine wa afya nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watoa huduma za fedha wapewa somo matumizi nishati mbadala

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirikisho la Asasi zinazotoa Huduma za Kifedha kwa Wajasiliamali (TAMFI), Winnie Terry, amewataka watoa huduma za kifedha kuwa na uthubutu na kujiamini kwenye kutoa huduma hizo kwa ajili ya nishati jadidifu.

Alisema hayo jijini hapa juzi wakati wa warsha ya matumizi bora ya nishati mbadala namna serikali inavyoshiriki katika mchango wa matumizi bora ya nishati jadidifu ikiwamo gesi na umeme jua.

"Nasema haya kwa sababu watoa huduma wadogo wa fedha wamekuwa wanasita kutoa huduma hizi za kifedha kwa ajili ya nishati endelevu kutokana na kuwa na wasiwasi. Wanatakiwa wajiamini," alisema.

Terry alisema matumizi ya nishati jadidifu yanaweza kunusuru uharibifu wa mazingira.

Pia alisema utoaji elimu na ubunifu ni moja ya mambo ambayo yanahitajika katika kuhakikisha watu wengine wanapata elimu juu ya nishati hiyo na matumizi yake ili kuondoa tatizo la uharibifu wa mazingira.

Alisema lengo la warsha hiyo ni kukutana na wadau mbalimbali wakiwamo wa nishati mbadala ili kubadilishana mawazo na kuzungumzia sera na taratibu zinazomgusa moja kwa moja mtoa huduma za kifedha. Alisema watoa huduma wadogo wa fedha wamekuwa wanasita kutoa huduma kifedha kwa ajili ya nishati endelevu .

"Tuliona ni vyema kukutana kwa pamoja kujadili haya mambo jinsi gani hizi taasisi za fedha zinaweza kuunganisha namna bora ya kutoa huduma katika suala zima la nishati jadidifu," alisema.

Mwezeshaji katika warsha hiyo, Finias Magesa, alisema wamejadili sera zilizopo za nishati jadidifu zinavyoweza kuleta ongezeko la nishati jadidifu kupitia ongezeko la huduma za fedha ambazo zinatolewa kwa kuwa kumekuwa na kusita sita kwingi kwa mashirika hayo.

"Sijui ni uelewa mdogo juu ya nishati jadidifu na jinsi ya kuzinufaisha hizi taasisi za fedha," alisema.

Aidha, Mwakilishi kutoka shirika la Simusolar, Raymond Anthony, alisema hatima ya yale waliyojifunza imewasaidia kuongeza idadi ya Watanzania ambao wanatumia bidhaa zao sababu mabadiliko ya tabianchi yaliyopo wakati huu yanawataka kuwa na uwezo wa kutumia mbinu mbadala kwajili ya uzalishaji pia kupata ulinzi na kipato cha mtu mmoja mmoja.



# Uamuzi wa pingamizi kesi ya vileo Januari mwakani

**Na Mwandishi wetu,**
ZANZIBAR

HATIMA ya kesi ya Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) dhidi ya Mwanasheria Mkuu na Bodi ya Udhibiti Vileo ya madai ya kuvunjwa Sheria Na. 9 ya Vileo ya mwaka 2020, itajulikana Januari 17, mwakani, baada ya hukumu kukwama kutolewa juzi na Jaji Abdulrakim Ameir Issa.

Katika kesi hiyo, JUMAZA wanadai kuwa Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar (ZLB) imevunja kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Vileo na kushindwa kusimamia masharti ya kifungu cha 28(k) kinachotaka baa kuwa umbali wa mita 1,000 kutoka makazi ya watu na huduma za jamii kama hospitali, nyumba za ibada, shule na madasrasa.

Wanasheria wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, wamefungua pingamizi wakidai kuwa kesi imefunguliwa kinyume cha sheria bila kutoa taarifa ya siku 60 ya kushtaki serikali pamoja na hati ya kiapo kutokuwa na tarehe.

"Leo ulikuwa utolewe uamuzi mdogo wa pingamizi la awali lakini Jaji anayesikiliza kesi amepata dharura badala yake hukumu itatolewa Januari 17," alisema Wakili wa JUMAZA, Omary Shehe.

Alisema katika kesi ya msingi, wanapinga uvunjwaji wa sheria unaofanywa na Bodi ya Udhibiti wa Vileo baada ya kutoa vibali kwa kampuni tisa za kuingiza vileo Zanzibar badala ya tatu, jambo ambalo ni kinyume cha sheria pamoja na baa kuendelea kupewa leseni za biashara kinyume cha sheria.

"Kifungu cha 28 (k) kinasema baa kabla ya kupewa leseni ya biashara, inatakiwa kuwa umbali wa mita 1,000 kutoka katika maeneo ya huduma za jamii kama makazi ya watu nyumba za ibada, shule na hospitali," alidai Wakili Omary.

Wakili huyo alidai kesi ya msingi ya JUMAZA bado iko pale pale licha ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuivunja bodi inayotuhumiwa kuhusika na kuvunja sheria katika utekelezaji majukumu yake.

Katibu wa Kamati ya Maadili ya Jumuiya ya Maimamu na taasisi za kiislamu Zanzibar, Sheikh Abdalla Mnumbi Abbas, alisema mahakama inapaswa kuharakisha kesi hiyo kutokana na kugusa maslahi ya umma.

Alisema kifungu cha 33(1) kimesisitiza wamiliki wa kampuni za uingizaji wa vileo kabla ya kupewa vibali lazima awe Mzanzibari, mlipa kodi, awe na ghala la kuhifadhia na gari kusambaza vinywaji badala yake wazungu wanaingiza pombe Zanzibar. Alisema kuna hadi hoteli za kitalii zimekuwa zikiingiza pombe kutoka nje ya Zanzibar bila kulipa kodi baada ya kununua kwa kampuni za ndani zenye vibali vya kuingiza vileo na kusababisha serikali kupoteza mapato.

Sheria namba 9 ya mwaka 2020 ilitungwa na Baraza la Wawakilishi, baada ya kujadiliwa Baraza la Mapinduzi (BLM) na kuanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais lakini Bodi ya Udhibiti wa Vileo imeshindwa kusimamia masharti ya sheria hiyo.

Kutokana na mabadiliko ya sheria hiyo, wamiliki wa baa wanatakiwa kulipia leseni Sh. milioni 4.8 badala ya Sh. milioni mbili wakati kampuni za uingizaji pombe zikitakiwa kulipia Sh. milioni 30 badala ya Sh. milioni mbili pamoja na gharama za ukaguzi Sh. milioni tano kwa mwaka.



RAIS wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi na Mkewe Mama Mariam Mwinyi wakisalimiana na kuagana na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja Idrisa Kitwana Mustafa na viongozi mbalimbali akiondoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar kuelekea jijini Dodoma kuhudhuria Kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, kilichotarajiwa kufanyika jana. **PICHA: IKULU**

## Waziri apigia debe muswada wa sheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wametakiwa kujipanga zaidi kuhakikisha wanachangia muswada wa kuanzishwa kwa mamlaka kamili ya kupambana na dawa za kulevya ili kuongeza kasi ya mapambano ya biashara hiyo haramu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Salum Mkuya, aliyasema hayo wakati akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu mswada wa kuanzishwa kwa mamlaka kamili ya kupambana na dawa hizo.

Alisema serikali imejipanga kupambana na uhalifu mbalimbali wa kimataifa ikiwamo matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya ambazo athari zake kwa nguvu kazi ya taifa ni kubwa.

Mkuya alisema kuwapo kwa mamlaka kamili ya kupambana na dawa za kulevya itakuwa na uwezo ikiwemo wa kukamata,kufikisha mahakamani pamoja na kufanya uchunguzi wa tuhuma hizo kikamilifu.

Alisema iliyopo sasa haijafanikiwa kwa kiasi kikubwa kupambana na kudhibiti dawa za kulevya huku ikiwapo mianya mingi inayotoa nafasi ya kuwapo uhalifu huo.

"Upungufu mwingi uliopo katika Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya ndio umesababisha kuja na marekebisho ya sheria ya kuwapo kwa mamlaka kamili itakayofanya kazi za uchunguzi, kukamata na kufikisha mahakamani," alisema.

Mkuya aliwaambia wajumbe kwamba serikali ya Zanzibar na ya Uingereza zimeingia makubaliano ambayo lengo lake kupambana na uhalifu ikiwamo wa dawa za kulevya.

Alisema kisiwa cha Zanzibar kimekuwa kikitumiwa na watu mbalimbali wakiwamo wahalifu kwa ajili ya kuingiza dawa za kulevya, hivyo serikali imekubaliana na Uingereza kuongeza mashirikiano yatakayodhibiti matukio hayo.

"Hizo ndizo sababu kubwa zilizoifanya Zanzibar kuingia makubaliano na serikali ya Uingereza katika kupambana na uhalifu ikiwamo wa kupambana na dawa za kulevya," alisema.

# SMZ yabainisha malipo kampuni iliyofilisika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Aboud Hassan Mwinyi, amewataka wananchi waliowekeza fedha zao katika kampuni ya Masterlife kwamba kiwango cha fedha watakacholipwa ni kile walichokiweka na si faida ya uwekezaji.

Aliyasema hayo jana wakati akikagua uhakiki na utoaji wa akaunti za benki kwa ajili ya wananchi walioathirika na kampuni hiyo awamu ya pili unaoendelea katika Shule ya Sekondari Haile Salassie.

Aboud Mwinyi alisema wananchi wafahamu kwamba serikali haitalipa kiwango cha faida kwa mtu aliyewekeza katika kampuni hiyo na kile kitakacholipwa ni alichoweka pekee.

Pia alisema serikali imeweka fedha za kutosha kwa ajili ya kuhakikisha kila mwananchi aliyeathirika katika kampuni hiyo anapatiwa fedha zake.

Naibu Katibu Mkuu alibainisha kuwa serikali imefanya zoezi hilo kwa mara ya kwanza kwa wananchi walioathirika kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja na tayari wote wameshalipwa fedha zao.

Alisisitiza kwamba wananchi wote wa awamu ya pili watalipwa kwa kutumia akaunti za akaunti na hakuna mwananchi atakayelipwa fedha taslim.

"Mpo hapa kwa ajili ya kuleta taarifa zenu za benki na tunazikusanya ili kuwalipa. Nyote mtapata fedha zenu muda si mrefu, hivyo uvumilivu ni muhimu. Lengo la serikali ni kuona kila mwananchi anapatiwa haki yake," alisema.

Aboud aliwatoa wasiwasi wananchi na kuwaahidi kwamba kila mtu ambae aliweka fedha zake katika kampuni hiyo atapatiwa bali kitu cha msingi ni kuwa wavumilivu na busara katika zoezi hilo.

"Tunawaombeni wananchi muwe wavumilivu kwani serikali yenu tayari kwa awamu ya kwanza imeshalipa wananchi walioathirika zaidi ya 4000 kwa mkoa wa Kaskazini kuanzia Sh. 100,000 hadi Sh. 1,000,000 nanyi mtalipwa kama wenzenu," aliahidi.

Kamishna wa Bajeti, Wizara Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Saumu Khatib Haji, alisema awamu hiyo ya pili ambayo inafanyika kwa mikoa yote ya Unguja, wananchi 3,558 ambao majina yao yamebandikwa katika maeneo husika wanatarajiwa kuhudumiwa na kupatiwa fedha zao.

Akizungumzia changamoto zinazojitokeza kwa awamu ya pili, alisema ni pamoja na wingi wa watu wanaohitaji huduma na kutaka kuhudumiwa wa kwanza.

Pia alisema changamoto nyingine ni mwananchi kwenda na mikataba ya watu 20 ambaye ni wakala, hivyo kwa sasa wamesitisha huduma kwa watu hao na kusisitiza wanaotaka kuwakilishwa suala lao litakuwa leo.

Kuhusu wananchi kupigiwa simu na kufunguliwa akaunti wakati wa ulipaji wa fedha hizo kwa awamu ya kwanza katika mkoa wa Kaskazini, alisema awamu hii suala hilo haijajitokeza na kwamba walilidhibiti mapema kwa kushirikisha benki.

Aliwashauri wananchi kuendelea kuiamini serikali yao na kuonyesha imani kubwa kwa Rais Mwinyi kwa imani yake ya kuwarejeshea fedha zao ambazo walitapeliwa.

"Serikali haikupanga kumdhulumu mwananchi kwa sababu serikali ni baba na wananchi ni watoto wake hivyo sio rahisi baba kumdhulumu mtoto wake na wengi wameona amana walizoweka wanaikuta kama waliyoiweka," alisisitiza.

Sambamba na hayo aliwasihi wananchi ambao bado hawajaona majina yao kuendelea kuwa wastahalimilivu kwani majina yapo na yatatolewa wakimaliza awamu hiyo.



**RAYVANNY**
UKURASA 12



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# KILI&NEEMA Dhahabu ya Kimasai inayong'ara India

DUNIA imehamanika baada ya vijana wawili kutoka jamii ya Kimasai, kutetemesha tasnia ya filamu kutokana na umahiri wao wa kuimba nyimbo mbalimbali za wasanii wakubwa wa Bollywood nchini India.

Hata hivyo, vijana hao Kili na Neema Paul kutoka kijiji cha Lugoba, wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, licha ya kutojulikana sana hapa nchini, hali ni tofauti huko India na mataifa mengine ambako wamekuwa maarufu na kuonekana kama mashujaa wao.

Wasanii wakubwa wa filamu wa Bollywood, wameshangazwa na vipaji vya vijana hao na kusababisha kufikiria kuwashirikisha katika baadhi ya kazi zao.

Kili na Neema wamefahamika na kuwa maarufu kupitia mitandao ya kijamii ya Tik Tok na Instagram, ambako wanapata nafasi ya kuonyesha kazi zao kwa kurudia nyimbo za wasanii wakubwa huku wakiwa katika mandhari ya kitamaduni ya Kimasai.

Kutokana na umaarufu wao, makampuni ya kimataifa yapo mbioni kuingia nao mikataba ya kibiashara kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wafuasi.

Akizungumza na vyombo mbalimbali vya habari, Kili amesema anamshukuru Mungu kwa umaarufu waliopata, lakini kwa sasa imekuwa kazi ngumu kwao kutokana na kutakiwa na wanahabari wengi kufanya mahojiano

"Vyombo vingi vya habari hasa nchini India wanataka kufanya mahojiano na sisi, imekuwa wakati mgumu sana lakini inapendeza kuona tunajulikana na tumevuka mipaka ya Tanzania," amesema Paul.

Hata hivyo, amesema siku si nyingi ndoto yake inaweza kutimia kutokana na kuwepo na mpango wa kufanya kazi na msanii mkubwa kutoka Bollywood na hivyo kuitangaza vyema Tanzania.

BASI SAWA

## Bongo muvi msaidieni Bambucha




ILE dhana kwamba wasanii wa filamu hawasaidiani inaweza kufutika endapo kilio cha mwigizaji Omary Said maarufu kama 'Bambucha' kitafanyiwa kazi.

Kwa sasa Bambucha hajiwezi baada ya kukatwa mguu na ameomba msaada wa kumudu matibabu wakati akiendelea kuangaliwa afya yake na wataalamu.

Kulingana na kituo cha runinga cha EATV, msanii huyo anaomba msaada wa kifedha ili kuweza kununua dawa, kusafisha mguu aliokatwa na matibabu mengine.

## Ibraah taratibu usije ukajifunga



MWANAMUZIKI wa kizazi kipya kutoka lebo ya Konde Gang, Music Ibraah Tz, amesema kamwe hategemei kiki kupata umaarufu, bali kazi nzuri anazofanya zinajiuza zenyewe.

Amesema kuandika nyimbo nzuri na zenye ujumbe sahihi na kweli ndio silaha kwa msanii anayejitambua, na kuacha tabia ya kushambuliana na kukoseana heshima bila sababu za msingi.

"Mimi nipo Konde Gang ninaamini kuwa na kazi nzuri ndio unapata umaarufu na siamini kiki katika maisha yangu, ni lazima kila mtu kutambua umuhimu wake na kuachana na mambo ya kushambuliana kwani hataleta tija katika sanaa," amesema Ibraah.



## Rayvanny utaufikia upendo wa Malaika?

MKALI wa muziki wa Bongo Fleva, Rayvann, ameshukiwa kama mwewe baada ya kudai wimbo wake 'Tetema' haujawahi kutokea tangu Tanzania ipate Uhuru.

Baadhi ya watu walioshiriki katika ukurasa wake wa Instagram, wamesema Rayvanny, hajafanya utafiti wa kina kujua kama wimbo huo ni wa kwanza kupendwa nchini na Afrika Mashariki, wamemtaka kurudi kwenye kumbukumbu kuangalia nyimbo gani zilitamba na zinaendelea kufanya vizuri hadi sasa.

"Rayvanny asidanganyike na watu waliotazama kupitia YouTube na akajisifu kwamba wimbo wake ndio pekee umefanya vizuri tangu uhuru, aende katika kumbukumbu zake akaangalie nyimbo kama Malaika au Rangi ya Chungwa, halafu atajiona kwamba yeye amekosea," amesema mdau mmoja.



## Barakah kubali kuachwa

MSANII wa Bongo Fleva, Barakah The Prince, amesema umbali wa sehemu wanazoishi yeye na aliyekuwa mpenzi wake Najma, umesababisha kuachana.

Barakah amesema yeye ameumbwa na wivu hivyo kuishi mbali kulisababisha kuhisi tofauti na kuwa na maswali mengi jambo ambalo liliwafanya wajadiliane na kutoa uamuzi wa kuachana na kubaki kama marafiki.

"Kuachana siyo jambo la ajabu katika mapenzi, mimi na Najma tulikubaliana kuwa tofauti kulingana na maisha yetu hasa umbali wa sehemu tunazoishi ambao unasababisha kuwa na migogoro mara kwa mara " amesema

## GUBU LA MUME: Gumegume lililoshindikana

**Na Adam Fungamwango**

MWANAUME ni kichwa cha nyumba. Huu ni msemo wa waswahili kuwa mwanaume ndiye anayebeba majukumu yote ya nyumbani ya kila siku. Mwanamke yeye ni msaidizi wake. Lakini mwanaume anatakiwa pia kuwa na tabia nzuri ili wanaokufuata, mke na watoto nao wawe na tabia hizo.

Baba akiwa na tabia mbaya, ni wazi pia anaowaongoza nao wataiga tabia hiyo.

Filamu ya 'Gubu la Mume' inaonyesha ni jinsi gani baadhi ya wanaume wamekuwa na tabia mbaya, ambazo hawakutakiwa kuwa nazo.

Baadhi ya wasanii waliocheza ni Zuberi Mohamed 'Niva' na Najma Mohamed. Inamuonyesha Niva kuwa anayeishi na mkewe Najma kuwa ni mwanaume mwenye gubu, mchoyo na tabia zingine zinazofanana na hizo.

Hataki ndugu yake yoyote na hata wa mkewe wafike nyumbani kwake. Tatizo lake kubwa ni uchoyo, kwani anaona wakija watakula chakula chake.

Pia amekuwa na maneno mengi na sheria nyingi kwa mkewe. Hataki avae nguo ambazo anaona mkewe atapendeza. Hataki aende saluni atengeneze nywele apendeze. Mke anakubaliana na hilo.

Lakini shoga yake mmoja anamuuma sikio na kumwambia asiwe anakubaliana na kila kitu anachosema mumewe na akaahidi kurekebisha hali hiyo. Kwanza akampeleka saluni Najma. Niva aliporudi akakasirika sana. Alipotambua kuwa ni shoga yake huyo alimfokea na kunyang'anya pesa. Kwa bahati mbaya sana mpenzi wa mwanamke huyo ni baunsa. Akaenda kusema kwa mpenzi wake. Niva akasakwa na kupatikana, akapigika hadi akasalimu amri.

Lakini akabakia na suala la uchoyo. Mjomba wa mkewe akaja kutoka kijijini, lakini na shangazi ya mkewe naye pia akaja.

Kitendo cha kukaa kwa mkwe wao kwa siku kadhaa



kilimkera mno Niva, kiasi kwamba hadi wakatambua kuwa hawatakiwi hapo na mkwe wao.

Wakaondoka. Siku waliporudi walikuja ukoo mzima na kumchukua ndugu yao. Mke naye alikuwa amechoshwa na visa vya mumewe, akaondoka, huku akitaka talaka ifuate nyuma.

Hili lilimuumiza sana Niva. Alimpenda sana mkewe. lakini tabia yake haikuwa na dawa. Alianza kuwa mlevi ili kupoteza mawazo. Akiwa kwenye mabaa, akaanza kazi ya kuwaelimisha wenzake juu ya kuishi vizuri na wake zao. Kuacha uchoyo na gubu.

## UHURU, WANAMUZIKI MIKONGENI TANGA

**Na Adam Fungamwango**

KABLA hata ya Uhuru wa Tanganyika, kwa sasa Tanzania Bara, sehemu za Tanga kuanzia Hale kuelekea Tanga mjini kulikuwa na mashamba makubwa ya mkonge ambayo yalihitaji wafanyakazi wengi.

Watu kutoka mikoa mbalimbali nchini walimiminika mikongeni kwa ajili ya kufanya kazi kwenye mashamba hayo. Kutokana na hali hiyo kulihitajika huduma za jamii kama zahanati, shule, baa na hata kumbi za burudani.

Hiyo ilisababisha wenye vipaji vya kupiga magita na kuimba, kutengeneza makundi ya kuburudisha na ndipo kulipoanzishwa makundi kama Atomic Jazz na Jamhuri Jazz ambayo awali ilijulikana kama Nyamwezi Jazz kutokana na wamiliki wa bendi kuwa ni watu kutoka Tabora.

Baada ya Uhuru mwaka 1961, majina yaliyoonekana ni ya kikabila yalipigwa marufuku na ndipo Nyamwezi ilipobadilishwa jina na kuitwa Jamhuri Jazz Band.

Wenye vipaji vya muziki, pamoja na kuburudisha wenzao, waliwafundisha watoto muziki, hivyo kutengeneza kizazi cha wanamuziki baada ya watu hao waliahamia.

Wazee hao walioangozwa na Mwanamasongi, walitengeneza vijana wengi waliokuja kuwa wanamuziki wakubwa nchini na Afrika Mashariki.

Hawa ni baadhi ya wanamuziki wakubwa tu ambao wametokea Tanga, na asili ya wazazi wao ni watu waliokuja kwenye kazi za mikonge.

**Wilson Peter na Geoge Peter Kinyonga**

Wanamuziki hawa ndugu ni baadhi ya wanamuziki ambao wametokea maeneo ya Hale mkoani Tanga.

Asili yao ni mkoa wa Kigoma na Rukwa walikotokea wazazi wao wakija kufanya kazi mikongeni.

Walitokea kuwa wanamuziki wakubwa Afrika Mashabiki, baada ya kuunda bendi ya Simba Wanyika nchini Kenya.

Kabla ya hapo walianzia Tanga kwenye bendi ya Jamhuri Jazz kwenye miaka ya '60, kabla ya kuelekea Arusha na kuvuka mpaka kuelekea Kenya ambako walipiga muziki kwa miaka mingi, wakafariki huko na kuzikwa huko mwanzoni mwa miaka ha '90.

**Tx Moshi William**

Ukimsikiliza Tx Moshi uimbaji wake, unafanana sana na George Peter wa Simba Wanyika. Ukweli ni kwamba Tx Moshi alimpenda sana mwanamuziki huyo na kuiga aina yake ya uimbaji.

Kwa mujibu wa Tx Moshi mwenyewe kabla hajafariki mwaka 2006, ni kwamba alicheza na George wakati wa utoto, huku Wilson akiwa mkubwa kidogo kwao.

Na wote walifundishwa muziki na mzee Mwanamasongi huko Hale mkoani Tanga.

Kwa upande wake wazazi wake walitoka Mwanza na mama yake akitokea Ruvuma.

Baada ya kutoka mkoani Tanga, alikwenda Dar es Salaam na kujiunga na Polisi Jazz, kabla ya kuchukuliwa na Juwata Jazz Band 'Msondo Ngoma'.

**Hamza Kalala**

Ni mpiga solo maarufu nchini. Wazazi wake wana asili ya mkoa wa Katavi kwa sasa.

Walikwenda Tanga kwa sababu ya kazi za mikonge. Yeye amezaliwa huko na kujifunza muziki, kabla ya kuwa mwanamuziki mkubwa nchini, akipigia bendi mbalimbali kama Uda Jazz, Vijana Jazz, Matimila, Washirika na Bantu Group.

**Hemed Maneti**


Ni mwanamuziki mwimbaji maarufu nchini aliyefariki dunia mwaka 1990 jijini Dar es Salaam akiwa ni kiongozi wa bendi ya Vijana Jazz.

Huyu naye ametokea mikongeni Tanga. Baba yake ni mzaliwa na Sumbawanga mkoani Rukwa na alikwenda huko na kufanya kazi ya udereva.

Alifundishwa muziki huko, lakini aliibukia mkoani Morogoro akiwa na Cuban Marimba, TK Lupopo na baadaye Vijana Jazz.

**Luza Elias**

Huyu ni mpiga saxophone maarufu nchini akitokea mkoani Iringa. Aliibuka kuwa mwanamuziki maarufu akiwa na bendi ya Jamhuri Jazz akiwa na kina Wilson Peter na George Peter na baadaye walimchukua kwenda naye Simba Wanyika, kabla ya kurejea nchini na kujiunga na Mwenge Jazz.




# Cardi B maliza mizungu yote

RAPA mkali wa Marekani, Cardi B, amedhihirisha kwamba bado ana mahaba mazito na mume wake Offset, na kamwe hakuna mtu atakayeweza kuwatenganisha.

Mwanamuziki huyo machachari wiki hii, alitupia picha kwenye ukurasa wa Instagram, akimpongeza mume wake kutimiza miaka 30, lakini aliwashtua wengi kutokana na aina ya mikao ya wawili hao iliyoonyesha wapo katika mahaba mazito.

"Nakutakia furaha ya kuzaliwa mume wangu mpenzi, nakupenda sana na huwa najivunia na natarajia mengi kutoka kwako," ameandika Card B.



## Tonto tulia kwanza mtamalizana wenyewe

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Tonto Dikeh na Chioma Ifemeludike, wametupiana maneno makali baada ya kuwepo na tofauti katika uchunguzi wa kifo cha mwanafunzi mmoja Slyvester Oromoni.

Oromoni alikuwa mwanafunzi wa chuo kikuu cha Dowen, ambaye alikufa baaada ya kupata ajali iliyomsababishia majereha makubwa.

Dikeh katika ukurasa wake wa Instagram, alipuuza uchunguzi huo na kuelezea kama wa kizembe jambo ambalo Chioma alipingana nalo na kumtaka aache vyombo husika vifanye kazi.

## Kim mbona kama hutaki unataka vile

MWANAMITINDO na mshiriki wa kipindi cha maisha cha televisheni, Kim Kardashian amesema ombi lake la talaka kutoka kwa Kanye West, lisiondoe utamaduni wao wa kuwa pamoja wakati wa Krismasi.

Katika video yake fupi aliyoiweka katika mtandao wa Tiktok, alionyesha soksi sita nyeupe, ikiwa pea mbili zake na Kanye West na nne kwa watoto wao North (8), Saint (6), Chicago (3) na Psalm (2) .

Katika video hiyo ambayo sasa imefutwa, nyota huyo wa televisheni alionyesha mapambo ya kifahari ya Krismasi nyumbani kwake.





## Dr Dre umeanza maisha ya usingo!

MWANAMUZI mkongwe wa Marekani, Dr Dre hatimaye amefanikiwa kumpa talaka aliyekuwa mkewe Nicole Young.

Kulingana na picha alizoweka katika mtandao wa kijamii, rapa huyo mwenye mafanikio makubwa ameonekana kuwa na furaha zaidi baada ya kupitia mchakato mrefu wa kutoa talaka.


Baadhi ya picha alionekana Dr Dre akiwa mbele ya bango kubwa lenye maandishi talaka huku akionekana kuwa na furaha kupita wakati wowote.

## Rapa auawa kwa risasi Marekani

MWANAMUZIKI wa Hip hop wa Marekani, Slim 400 ameuawa katika tukio la kupigwa risasi na mtu asiyejulikana.

Rapa huyo na msanii mwingine walipigwa risasi wakati alipofika nyumba ya jirani karibu na kwake siku ya Jumatano, na mtu ambaye hajafahamika bado.

Slim 400 amekuwa na matukio kadhaa ya kunusurika katika kifo, na tukio la kukumbukwa ni lile la 2019 kushambuliwa wakati akienda kujulia hali familia yake katika mji wa Compton .



# Prof. Mkumbo: Biashara ya uhakika siku zote iko kwa mama, kwa baba ...

## •Bosi TGNP amdokeza kazi inavyoendelea

**Na Yasmine Protace**

TAREHE 10 mwezi huu ndio ilitamatisha Maadhimisho ya Siku 16 Kupinga Ukatili wa Kijinsia. Pia ni siku ambayo duniani kunaadhimishwa Siku ya Haki Duniani, vivyo hivyo siku moja kabla ilikuwa kilele cha Maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa nchi, Desemba 9.

Katika nyendo za siku hizo 16, asasi ya TGNP Mtandao ambayo iko mstari wa mbele katika maadhimisho hayo, iliandaa matukio mbalimbali yaliyokamatwa na mijadala ikiwajumuisha watendaji waandamizi wa kiserikali kujadili hoja, wakiwamo mawaziri.

Wakati wa hafla ya kilele husika, mwalikwa alikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, na anaanza kwa kuwasifu kinamama akitaja katika eneo lao la biashara ndio kunafanyika vizuri na kudumu, akitoa ulinganishi kwa wanaume huwa hazifiki mbali au hata zinakufa.

Anasisitiza katika masuala ya uchumi wanawake ni muhimu akitaja takwimu, asilimia 90 ya pesa za biashara wanazozipata kinamama zinatumika kwa mahitaji ya nyumbani kama vile kodi za nyumba na matumizi ya chakula.

Prof. Mkumbo anaongeza kuwa masuala ya kijinsia ni ya kuzingatiwa sana akitoa mfano katika Umoja wa Ulaya, usawa wa kijinsia upo na wanawake ni wengi katika uongozi, hivyo anasisitiza masuala yanayomundolea utu mwanadamu hayapaswi kufumbiwa macho, ndani ya harakati za kupambana na ukatili wa kijinsia.

Katika suala la soko kuwa na vyumba kwa ajili ya wafanyabiashara kuwanyonyeshea watoto wao, ambayo ni sehemu ya ombi walilofikishiwa serikalini, Prof. Mkumbo anawajibu atawasiliana na wataalamu husika ufanyike mchakato wa kupatikana vyumba vya kuwasaidia wanawake kuwaweka watoto katika mazingira salama.

Prof. Mkumbo aliyekuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, anasisitiza haki, uhuru na usawa ni vitu vya kuzingatiwa, akitamka: "Wanyama ndio hawana usawa, uhuru na haki na ndio maana tumekuwa tukiwachinja."

**TGNP& MDAU MGENI**

Hellen Fish, mdau kutoka asasi ya Global Health ya Canada, anataja usawa kijinsia unabeba pia dhana ya kukomesha unyanyasaji kwa wanawake na wasichana.

Anatoa mfano wa serikali ya Canada, sasa iko katika mwaka wa 30 tangu kuanzisha msukumo wa usawa wa kijinsia, ikiwamo kuwawezesha wanawake na wasichana.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi anachangia hoja akisema katika maadhimisho ya kila mwaka, TGNP imejikita katika tathmini ya utengwaji fedha za utekelezaji Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).

Anasema mbali na kusherekea hatua zilizofikiwa na serikali katika utekelezaji wake kwa kutenga fedha, pia inajadili namna ya kutatua changmoto zilizopo na kuweka mikakati ya pamoja ya kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini.

Lilian anasema serikali kwa kushirikiana na wadau, iliandaa MTAKUWWA wa kutekelezwa kati ya mwaka 2017 hadi 2022, ukilenga kutokomeza kwa wanawake na watoto kwa asilimia 50, ifikapo mwaka huo 2022.

"Katika kufikia azma hiyo, mpango ulibainisha maeneo mahususi manane ya utekelezaji.



Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi.

Maeneo hayo ni kuimarisha uchumi wa kaya,mila na desturi, mazingira salama katika maeneo ya umma, malezi na msaada kwa familia, uhusiano, utekelezaji na usimamizi wa sharia, utoaji huduma kwa waathirika wa ukatili, mazingira salama shuleni na stadi za maisha, pia uratibu, ufuatiliaji na tathmini," anasema

Mbali na vyanzo vingine, anaitaja programu ya TASAF, kuna jumla ya Sh. 107,916,895,450 zilitumika kusaidia utekelezaji mbalimbali, ikiwamo kuongezeka vituo vya mkono kwa mkono vilivyoanzishwa kitaifa, ili kurahisisha utoaji huduma kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia.

Anataja baadhi ya vituo hivyo, vingi vikiwa katika hospitali mbalimbali za miji, baadhi yake ni Amana na Mwananyamala (Dar es Salaam), Tumbi (Kibaha), Iringa, Tabora Kitete, Sekou Toure (Arusha), Mbeya FFU, Simiyu, Shinyanga, Kahama, Hai, Mount Meru (Arusha) na Nindo, Shinyanga .

Lillian anafafanua: "Jumla ya nyumba salama sita zimesajiliwa mkoani Arusha (Faraja), Kigoma (Wote Sawa), Mara (Hope for Girls & Women in Tanzania na ACT Mara), Kilimanajaro (Network Against Female Genital Mutilation) na Manyara (Masai Girls Rescue Center)."

Pia anataja kuwapo madawati ya jinsia 420 katika vituo vya polisi mbalimbali nchini, huku wakihamasisha wanaokumbwa na ukandamizaji wa madhila hayo wajitokeze kutoa ufafanuzi.

"Hadi Februari 2021, jumla ya simu 1,079,891 zilipokewa na kufanyiwa kazi. Takribani wahanga 5,228 walipatiwa huduma ikiwamo kupelekwa kwenye nyumba salama, huduma za kisheria na ushauri nasaha, ukilinganisha na mwaka 2019/2020 ambayo ilikuwa ni wahanga 3,044 tu," anasema .

**MALEZI/MSAADA FAMILIA**

Lilian anasema katika eneo la malezi, msaada kwa familia na uhusiano hatua imepigwa na serikali kwa kushirikiana na wadau kukianzishwa jumla ya mitandao ya malezi chanya 3,963 katika jamii katika mikoa mbalimbali nchini, ikilinganishwa na mwaka 2019/2020 kulianzishwa mitandao 2,777, inayotumika kufanya majadiliano ya rika, ikilenga kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Lilian anasisitiza kuwa jinsia ni suala la maendeleo na kwa mantiki hiyo, TGNP imeamua kuandaa kongamano kuwa sehemu ya kutoa fursa, wadau wengine kutafakari wapi wamefanikiwa, penye changamoto na kupanga mikakati ya kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini, kupitia utengwaji rasilimali zinazotosha.

## TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Maisha ya umwamba yalivyoteka soka la mchangani hadi dansini

## ●Kila eneo timu za wababe, dansini getini

Na Adam Fungamwango

USHINDANI kwenye soka la mitaani kwa sasa umepungua sana tofauti na huko miaka ya nyuma.

Na hata utemi kama ule wa zamani siku hizi haupo kutokana na ustaarabu kuzidi kutamalaki, pia na teknolojia, ikiwamo vituo vingi na polisi.

Zamani mtemi mmoja anaweza kusimama njiani na kukataza mtu yoyote kupita upande mmoja kwenda mwingine kwa hata saa mbili na hakuna yoyote atakayemfanya lolote hadi aamue mwenyewe.

Hata unashindwa kujiuliza utemi wa aina hiyo ulikuwa unawasaidia nini.

Halafu kila mtaa, au eneo lolote kama stendi, sokoni hadi shuleni kulikuwa na mtemi maalumu, tena shule wakienda mbali kuiga, kuna mtemi wa darasa hadi mtemi wa shule.

Tukirudi kwenye soka, ni kwamba miaka ya nyuma kulikuwa na ushindani mkubwa kwenye timu ndogo tu za mitaani ambazo zilikuwa na mashabiki kindakindaki kama wa Simba na Yanga. Wako tayari kufia timu. Wake kwa waume walichanga pesa kuhakikisha timu yao inaingia michuano fulani, inasafiri, inakula na wachezaji wanapata posho.

Mfano timu ya Boom na Ashanti za Ilala. Hizi timu zilikuwa na upinzani wa jadi unaofanana kabisa na ule ya Simba na Yanga. Zikicheza kwenye Uwanja wa Karume, Dar es Salaam, Ilala nzima inakuwa baridi siku hiyo. Watu watamiminika kwenda kushuhudia mechi hiyo, ambayo kama ikiisha salama bila kuvunjika, au mashabiki kutopigana, ni bahati kubwa.

Haikushangaza ndiyo mechi iliyokuwa ikilindwa na askari wa kikosi cha mbwa na farasi, mithili ya mechi ya Simba na Yanga. Nadhani ndiyo mechi pekee iliyokuwa na ulinzi mkali zaidi kuliko yoyote ile ukiondoa Simba na Yanga.

Ukiacha timu hizo, Dar es Salaam nzima kulitapakaa timu mbalimbali za mitaani ambazo pia zilikuwa na mashabiki wake. Baadhi ya mashabiki walikuwa ni watemi wa timu ambayo siku hizi wanaitwa mabaunsa.

Lengo la watemi hao ni kuhakikisha wachezaji na mashabiki wanakuwa salama wanapokwenda kucheza michuano ya makombe mbalimbali na kurejea salama.

Mara nyingi michuano ya zamani ilikuwa ya kitemi zaidi, hata baadhi ya waamuzi walilazimika kuchezesha wakiwa na visu, mapanga na bisibisi. Baadhi walikuwa pia wachezaji karate, fani iliyofifia sasa.



Mwamuzi maarufu wa soka la mchangani, Dar es Salaam, Kipunje, akijiandaa kuchezesha mechi.

Haikuwa rahisi kwa mwamuzi mnyonge mnyonge kuchezesha mechi ya makombe mbalimbali wakati huo. Vinginevyo dhahama inaweza kumkumba.

Zipo timu zilizosifika kwa utemi uliopitiliza wakati huo, ikiongozwa na Kiboko Msheli ya Magomeni Makuti. Timu iliyotoa wachezaji wengi waliocheza Ligi Kuu kama Kessy Ramadhani 'Patel' aliyeichezea Sigara wakati huo ikiwa Ligi Kuu na wengineo.

Ni timu ambayo ilikuwa na watemi walioshindikana, kiasi kwamba siku ikicheza, wananchi wengi wa mitaa ya Magomeni, Mwanayamala, Tandale mpaka Kijitonyama ni lazima wajue ratiba ya mechi za timu hiyo. Siyo kwamba waende wakaishangilie, bali siku hiyo ikifika saa sita waanze kufunga maduka, biashara zao na wengine wawe majumbani ili wasikutane na kundi la mashabiki wa timu hiyo wanapokwenda kucheza mechi au kutoka kwa sababu kila watakaekutana naye, au kukutana na kitu chochote ni halali yao.

Timu zingine ni Manyema Rangers ambayo ilicheza mpaka Ligi Kuu, Kumkoma Nyani Giladi, mitaa ya Msasani kulikuwa na Liraida na Kambarage, kule Temeke kukawa na OPEC, Panama, Undundu, British, Mkenge Majini, Tandika walikuwapo Akatoko na Black September.

Mortuary Mob, Flamingo, Bonde FC, Zamalek, Taxi Bubu, Bicco, Mwananyamala Sports, zilikuwa ni timu za Mwananyamala.

Kigamboni kulikuwapo na timu za Nanga FC, Shabab, Tipper na Mzizima, Sinza kukawa na timu ya Abajalo ambayo alikuwa akichezea mtoto wa mwanamuziki maarufu nchini, Dk. Remmy Ongala, Kalimangonga Ongala au Kally Ongala.

Huyu aliichezea mpaka Yanga.

Magomeni kulikuwa na Wonder Boys, Linea Messina au Messina Line, Sheffield Wednesday, na Kiyungi FC ambayo alikuwa akichezea mtoto wa mwanamuziki mwingine maarufu nchini, Hemed Maneti, akiitwa Maneti Hemed.

Mikoani nako kulipamba moto, kwani Iringa kulikuwa na timu ya mtaani maarufu ikiitwa African Wonderers, Mbeya kulikuwa na Jogoo Baba, Tabora kukawa na Tindo ambayo alitoka Said Mwamba 'Kizota', Morogoro mjini pale viwanja vya Kichangani usiseme!

Kwenye timu hizo, kulikuwa na makamanda wa wababe ambao mara nyingi akifika uwanjani, kwanza anakuwa na dalili zote za ulevi, pili huwa hawaangalii mpira, badala yake wanazunguka kutafuta 'nani anajifanya mjanja'. Kuna mwingine anakaa kimya kwenye kona fulani kakunja uso, kuonyesha ishara zote yeye ni taifa kubwa. Huwa hawapendi timu zao zifungwe, wala wachezaji wao wababaishwe kwa hali yoyote ile.

Hata watemi wadogo wadog0 wapinzani waliwagwaya.

Hapo ndipo ukienda kwenye timu kama Liraida humkosi Zabaga na mwenzake mmoja, hali kadhalika, ukisogea Bonde FC, unakutana na Baraza, Messina Line kuna pande la mtu mrefu anaitwa Kala Shujaa ambaye alikuwa maarufu katika kila kipengele cha Magomeni hadi Manzese na bonde la Mburahati.

Hizo ni baadhi ya timu za mitaani ambazo zilitamba kuanzia miaka ya 1970 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000, timu nyingi zilipoanza kufa vifo vya asili au kupungua nguvu.

**DANSINI NAKO?**

Kwenye muziki nako ni hivyo hivyo. Kutokana na kuwa na watemi wengi wakati huo ambao walikuwa wakienda kufanya fujo hadi madansini, milangoni wakatafutwa watemi zaidi yao ili kukabiliana nao.

Msondo Ngoma ilikuwa na Chivalo na Dhahama ambao ni wazuia gadhabu mlangoni na DDC Mlimani Park, Sikinde Ngoma ya Ukae yenyewe wakaa milangoni wake walikuwa Chuma na Kitwana.

Hao kwa vile walikuwa waajiriwa, nao staili yao muda wote kununa mlangoni, akifuatilia kama taratibu zinaenda kwa usahihi, ole wako uende kinyume na utaratibu.

Hatua ya kwanza anakukunja, kukuhoji sentesi moja tu, au wakati mwingine akielekezwa anakuelekeza nje moja kwa moja bila mjadala na ole wako uje na kipengele cha kubishana, hapo utajua kigezo kilichofanya aajiriwe.

Mbali na kazi ya kukaa milangoni ili kila anayeingia dansini awe amekata tiketi, pia waliwalinda wanamuziki na kadhia yoyote ile ambayo itawakuta.

Uongozi wa bendi na wanamuziki waliwahusudu kweli kweli, kwani kila walichokitaka kiliienda sawa, hata kuwapa hadhi ya wanafamilia.

Ushahidi hai ni kwenye wimbo wa 'Uzuri si Shani', Juwata Jazz Band, Chivalo na Dhahama walipaishwa kwenye orodha ya wanamuziki waliotajwa, huku Sikinde iliponzishwa tu, vibao vya mapema, Chuma na Kitwana walitajwa kwenye wimbo wa 'Tufurahi na Sikinde'.

*** Maoni sms: +255 716 350534**



Mashabiki wa soka la mchangani, na mbwembwe zao, ambao mara nyingi mabaunsa ama wao, au wa upinzani hawako mita nyingi kutoka waliko. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

## Watu wafurahia kifo cha mke wa Pinochet

**SANTIAGO,** CHILE

UMATI wa watu umekusanyika katika mji mkuu, Santiago,nchini Chile wakifurahia taarifa ya kifo cha mke wa aliyekuwa rais wa taifa hilo Augusto Pinochet.

Lucia Hiriart, mjane wa dikteta Pinochet alifariki akiwa na umri wa miaka 99.

Katika kipindi cha dakika chache baada ya kutangazwa kwa taarifa hiyo, umati mkubwa wa watu walikusanyika katika mitaa mbalimbali ya mji huo kusherehekea kutokana na kuchoshwa na kile wanachoamini mwisho wa utawala wakurithishana.

Hata hivyo, baadhi wanamuona Hiriart kama mfadhili wa watu wasiojieweza. Lakini kwa wengine alijulikana kutokana na ushawishi wake kwa mume wake Pinochet.

Pinochet aliiongoza Chile kati ya mwaka 1973 na 1990, wakati huo watu zaidi ya 3,000 waliuawa au kutoweka.

Kifo chake kinakuja huku uchaguzi wa urais ulioigawanya nchi ukitarajiwa kufanyika Jumapili.

Wapiga kura watachagua baina ya kiongozi wa zamani wa wanafunzi Gabriel Boric, na mgombea wa mrengo wa kushoto aliyelaani utawala wa kijeshi uliopita wa Chile, na mgombea mwenye itikadi za mrengo wa kulia , Jose Antonio Kast.

**BBC**.

## Marekani kuwatimua wanajeshi 20,000

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeanza kuchukua hatua za kinidhamu kwa maaskari wake ambao wamekataa kuchomwa chanjo iliyoidhinishwa katika kujikinga na ugonjwa wa COVID-19.

Jumla ya wanajeshi 20,000 ambao hawajachanjwa wanakabiliwa na hatua kali ya kuachishwa kazi baada ya kukataa kupata chanjo hiyo.

Alhamisi, kitengo cha jeshi la wanamaji kilisema kimewasimamisha kazi askari 103 ambao hawakupata chanjo hiyo, huku jeshi la nchi kavu likiwachukulia hatua za kinidhamu zaidi ya wanajeshi 2,700.

Hata hivyo, taarifa zilisema mchakato wa kuwaachisha kazi utaanza mwezi Januari mwakani.

Awali jeshi la anga lilisema kuwa wanajeshi wake 27 waliachishwa kazi kwa kukataa kutii agizo hilo la kupata chanjo. Kwa miezi kadhaa sasa, viongozi wa kijeshi wamekuwa wakionya kwamba wanajeshi watachukuliwa hatua iwapo hawatafuata kile kinachochukuliwa kuwa agizo la kisheria la kupata chanjo hiyo.

**BBC**

# Mwanafunzi achomwa moto alazimishwa kuabudu shetani

**OSUN,** NIGERIA

WANAFUNZI katika Chuo Kikuu kimoja nchini Nigeria kilichopo mji wa Osogbo, jimbo la Osun wamemchoma moto mwenzao katika ibada za kishetani.

Msemaji wa polisi katika jimbo hilo, Yemisi Opalola, amethibitisha tukio hilo na kueleza lilitokea Desemba 11 mwaka huu.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na Chuo hicho, mwanafunzi huyo alikuwa na kiwango cha juu cha uelewa wa masomo, jambo lililomsababisha kulazimishwa na wenzake kuingia katika dini ya kuabudu shetani.

Msemaji wa chuo hicho Ademola Adesoji, alisema tukio hilo lilifahamika baada ya mwanafunzi huyo ambaye anafahamika jina Victor Oke, kukosa kuhudhiria mitihani yake ya masomo.

walipowasiliana na wazazi wake walieleza mtoto wao alishambuliwa na wanafunzi waliomlazimisha kujiunga na ibada za miungu, jambo ambalo hakulitaka.

"Walimpiga kwa mawe, wakapasua mwamba kwa mawe na kumchoma kwa moto kabla ya kuokolewa na watu ,"ilisema taarifa.

Katika mitandao ya kijamii nchini Nigeria watu wanashirikisha umma picha inayoonyesha Victor akipigwa.

Anaonekana kwenye picha moja akiwa ameketi ndani ya maji huku watu wakimpiga, na baadaye kumtupa kwenye moto uliokuwa umewashwa.

Victor alisikika akipiga mayowe akisema hataki kuabudu miungu.

Hata hivyo, mwanafunzi huyo yupo hospitali akipatiwa matibabu baada ya kutokea tukio hilo.

**BBC**



Wanajeshi wa Urusi wakiwa na kifaru karibu na mpaka wake na Ukraine hivi karibuni **(PICHA: DW)**

# Baraza la Usalama laijadili Ethiopia

**NEW YORK,** MAREKANI

BARAZA la haki za binadamu la Umoja wa Mataifa, litatarajiwa kufanya kikao cha dharura kwa ajili ya kujadili mzozo wa Ethiopia.

Wakati kikao hicho kinafanyika, taarifa zinadai kuna ongezeko la maafa katika jimbo la Tigray.

Kikao hicho cha Ijumaa, ambacho kiliombwa na Muungano wa Ulaya, kitaamua iwapo utateuliwa ujumbe wa kimataifa kuchunguza ukiukwaji wa haki za binadamu ambao makundi ya haki za binadamu yanasema unaweza kuwa uhalifu wa kivita.

Mzozo katika jimbo la Tigray uliibuka mwezi Novemba mwaka jana, wakati serikali ya Eritrea ilipotuma vikosi vyake ndani ya jimbo hilo kuzima mashambulio ya wanamgambo wa Tigray People's Liberation Front (TPLF) baada ya kuteka ngome za jeshi la serikali kuu.

Mwezi uliopita Umoja wa Mataifa ulitoa ripoti ya kurasa 100 iliyoelezea ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu katika jimbo la Tigray.

Baadhi ya vitendo hivyo ni ufyatuaji makombora katika miji, kuwauwa kwa raia na unyanyasaji wa kingono.

Wiki hii, mashirika ya haki za binadamu ya kimataifa, Amnesty International na Human Rights Watch yaliainisha maafa zaidi ikiwa ni pamoja na kuwafunga mahabusu watu wengi, ukatili, kuwalazimisha watu wengi wa jamii ya Watigrayan kuhama makazi yao.

Hata hivyo mashirika ya Umoja wa Mataifa hayana uwezo kwa kiasi kikubwa wa kuzifikia jamii nyingi ambazo zinakabiliwa na ukosefu wa chakula.

Muungano wa Ulaya (EU) ulisema Baraza la Umoja wa Mataifa la haki za binadamu lina jukumu la kuzuwia ukiukaji wa haki za binadamu, na kuhakikisha haki inapatikana kwa waathiriwa na nchi wanachama wa baraza hilo liteuwe wachunguzi wa kimataifa.

Hata hivyo, Ethiopia imepuuza hatua hiyo ikiitaja kuwa yenye uchochezi wa kisiasa.

**BBC**

# TASWO wapongeza wizara kugawanywa

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Wataalamu na Wanataaluma wa Ustawi wa Jamii Tanzania (TASWO) kimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kuitenganisha Idara ya Maendeleo ya Jamii na Afya. Pongezi hizo zilitolewa jijini Dar es Salaam jana na Mwenyekiti wa TASWO, Awadh Mohamed, akisisitiza kuwa hatua hiyo itasaidia utekelezaji wa majukumu ya idara hizo mbili kwa kuwa zimebeba majukumu makubwa.

Alisema utekelezaji, ufuatiliaji, usimamizi na uratibu wake umekuwa na vikwazo katika kuwafikishia huduma bora za ustawi wa jamii wananchi hasa makundi maalumu na watu wenye uhitaji maalumu, hali inayosababisha kukosa kizazi chenye usawa kama ambavyo Rais Samia alivyoeleza katika hotuba yake ya juzi.

"Katika idara kuu ya maendeleo ya Jamii kwenye awamu ya sasa kumekuwa na majukumu mengi zaidi mbali na afya ikiwamo huduma za ustawi wa jamii ambazo ni kubwa kwa majukumu yake," alisema.

Mohamed alisema huduma za ustawi wa jamii zimekuwa ni huduma mtambuka tangu uhuru na zimekuwa ni huduma muhimu katika kuzuia matatizo ya kijamii yanayoweza kuathiri jamii na hasa makundi maalumu.

Alisema kuwa kwa miaka mingi sekta ya ustawi wa jamii nchini haijapewa nafasi inayostahili kimuundo na hivyo kuathiri huduma za ustawi wa jamii kwa makundi yote yaliyotajwa licha ya kuwa na sera, sheria na miongozo mbalimbali inayoongoza utoaji wa huduma hizo.

"Kwa mfano kutokuwapo na idara kamili ya ustawi wa jamii katika ngazi ya halmashauri kumesababisha kukosa kifungu maalumu cha kupangiwa bajeti ya kutosha.

"Kumekuwa na changamoto ya kuwasilisha masuala ya ustawi wa jamii kwenye timu ya menejementi ya halmashauri kwa ukamilifu," alisema Mohamed.

Alisema kutenganishwa kwa sekta hiyo kunatoa fursa kwa sekta ya ustawi wa jamii kupewa uzito wa kipekee kuanzia ngazi ya taifa hadi mamlaka za serikali za mitaa na kujenga kizazi chenye usawa kama yalivyo malengo ya Rais na malengo ya dunia.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza katika kikao cha wataalamu kutoka wizara hiyo na wawekezaji wa kampuni ya Tree Global juzi jijini Dodoma. Mkutano huo ulifanyika kwa lengo la kuingia makubaliano kati ya serikali na kampuni hiyo katika upandaji wa miti ya korosho na kokoa ili kutunza mazingira na kupunguza umaskini. **PICHA: WIZARA YA KILIMO**

# Ng'ombe wanaodaiwa kufa kwa kula majani ya sumu wazua hofu

**Na Dege Masoli,** KILINDI

VIFO vya ng'ombe 17 kati ya 27 wanaodaiwa kula majani yenye sumu katika Kitongoji cha Mbogo, Kata ya Negero wilayani Kilindi, wamezua hofu kwa wafugaji, wakiiomba serikali kuingilia kati haraka ili kuepusha madhara zaidi.

Wakizungumza na NIPASHE jana, wafugaji hao, akiwamo Tembo Kirika na Marsaji Pereji, walidai ng'ombe hao walilishwa sumu wakati wakirejea nyumbani kutoka malishoni juzi jioni.

Tembo alidai wakati wachungaji walipokuwa wakirudi nyumba, walipofika kwenye kitongoji hicho, waliwaona ng'ombe wakianguka na kutoka povu mdomoni.

"Asubuhi wachungaji walitoka na ng'ombe hao kama kawaida lakini majira ya jioni nilipata simu ikinifahamisha kuhusu tukio hilo na tuliondoka kufika eneo la tukio tuliwakuta ng'ombe 27 wakiwa hoi, tulifanikiwa kunusuru 10 tu," alidai.

Pereji alidai kuwa ng'ombe hao wanahisi wamekula sumu kutokana na ukweli kwamba waliowahishiwa dawa walikuwa wakitapika sumu hiyo huku waliokufa walitoka povu mdomoni.

Mwenyekiti wa Wafugaji hao, Loata Elmedili, aliiomba serikali kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini watu waliotenda unyama huo kwa kuwa huenda wakasababisha migogoro ya kijamii.

Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Kilindi, Seleman Mwarabu, akizungumzia tukio hilo, alisema tayari wameanza kuchukua hatua ikiwamo kupata vipimo ambavyo vitawezesha kujua sababu za vifo vya mifugo hiyo.

Mwarabu aliwataka wananchi kuwa wavumilivu hasa yanapotokea matukio kama hayo huku akisisitiza umuhimu wa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria pale inapotokea jambo lolote linaloashiria uvunjifu wa amani.

# RC ataka uchunguzi wa matumizi fedha UVIKO

**Na Mary Mosha, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi katika ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano ya UVIKO-19 katika Manispaa ya Moshi baada ya kutembelea na kutoridhishwa na ujenzi huo.

Kagaigai alitoa agizo hilo juzi baada ya kutembelea vyumba hivyo vya madarasa, alisema licha ya Manispaa kupewa zaidi ya Sh. milioni 80 bado ujenzi huo hauridhishi.

"Ninatoa siku saba kufanya uchunguzi wa kina kwenye mikataba ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa kwenye Manispaa ya Moshi, ambavyo vimegharimu Sh. milioni 80 na kuangalia thamani ya fedha kama inaendana na hadhi ya jengo," aliagiza.

Akikagua ujenzi katika Shule ya Sekondari Anna Mkapa, Kagaigai alieleza kutoridhishwa na ujenzi katika vyumba viwili vya madarasa ambavyo vilikuwa na upungufu katika kuta, sakafu na milango ya madarasa.

"Sijaridhishwa na kuta, sakafu na mlango wa darasa hili. Kamanda wa TAKUKURU ninakupa siku saba uniletee taarifa za ukaguzi utakaofanya shule hizi mbili lakini pitia na nyingine ili kujiridhisha," alisema.

Mkuu wa Mkoa pia alishangazwa na hatua ya Mkurugenzi wa Manispaa Moshi, Rashid Gembe, Meya wa Manispaa, Juma Raibu, kutetea taarifa alizoziita potofu zilizokuwa zikitolewa na Mhandisi wa Manispaa, Richard Sanga.

Wiki iliyopita Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mkoa ilitembelea vyumba hivyo vya madarasa na kutokuridhishwa na hali ya ujenzi wa vyumba hivyo na kuagiza marekebisho yafanyike.

"Sijaridhishwa na hali ya ujenzi wa vyumba vya madarasa hasa kwenye mlango, sakafu na baadhi kuta. Kamati ya siasa ya wilaya hakikisheni mnakuja hapa kabla madarasa haya kabla hayajakabidhiwa," alisema Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, wakati wa ziara hiyo.

Wakizungumzia hatua hiyo, baadhi ya wazazi wa Manispaa ya Moshi, akiwamo Seleman Ramadhan, walisema ni wajibu wa viongozi wa serikali kufuatilia na kuona namna ambavyo ujenzi unaendelea katika vyumba vya madarasa ili kuepusha kuwapo kwa maafa.

"Hii ni hatua nzuri mkuu wa mkoa amechukua, hatujui kwa nini watu wameharibu, huu ni uharibifu wa fedha iliyotolewa na serikali," alisema Seleman.

## HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao walikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani nampenda kwa dhati. Alayempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-5

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Hujambo wewe."

"Sijambo nani mwenzangu?"

"Ina maana hukusevu namba yangu mwanaume wewe?"

"Mhhh inawezekana nilikosea kusevu."

"Mbona mimi nimekusevu na sijakosea?"

"Dada 'angu wee, mjini hapa, inawezekana nimekosea kwa sababu ya kuwaza mambo mengi kichwani." Ni jibu ambalo nusura limpasue mbavu Diana.

"Naitwa Diana, umenikumbuka?"

"Diana, Diana, Diana, yule ambaye siku ile pale aliporwa mkoba Mwananyamala A?"

"Hujakosea, ndiyo huyo huyo."

"Heee, jamani Mungu mkubwa, maana ni kweli ulinipa namba, lakini niliisevu vibaya, nikawa sijui tena namba yako na sikuwa na uhakika wa kuipata tena. Nilihuzunika sana. Nikasema nitampata wapi tena yule dada? Nitapata wapi tena namba yake. Nikaona ndiyo basi tena siwezi kuwasiliana nawe au kukuona tena."

"Kwa nini, mbona mimi nilichukua namba yako Jan?" Aliuliza Diana, lakini alichosikia ni kicheko kifupi kutoka kwa Jan.

"We huwajui wanawake warembo kama wewe. Yaani achukue namba aanze kukupigia kama ulivyofanya wewe hivyo. Ni nadra sana. Na hii nimeiona kwako tu dada."

"Yaani umenifanyia mema yote yale, halafu nikutupe, hata nisikusalimie?"

"Nakwambia hivi dada 'angu, wanawake wengi warembo hata umuokoe kwenye ajali ya ndege, akachukua namba zako, wewe usiwe na za kwake, anaweza hata asikupigie." Ikawa sasa ni zamu ua Diana kuangua kicheko.

"Yaani nimeshangana kunipigia wakati tayari namba zako nimeshapoteza, vipi kwema huko?"

"Kwema, nimekupigia kwanza ili nikushukuru kwa dhati, kwa sababu siku ile bado nilikuwa nimechanganyikiwa, akili yangu ilikuwa haijakaa sawa. Pili nilikuwa nataka uje nyumbani."

Hilo la kwenda nyumbani lilimshtua Jan. Hakutegemea. Msichana mrembo, anayeonekana anatoka kwenye familia yenye uwezo kidogo kuliko yake. Aliona ni kitu ambacho




**"Nakwambia hivi dada 'angu, wanawake wengi warembo hata umuokoe kwenye ajali ya ndege, akachukua namba zako, wewe usiwe na za kwake, anaweza hata asikupigie." Ikawa sasa ni zamu ua Diana kuangua kicheko.**

watoto wa mjini wanasema kwenda 'kujichoresha'.

"Yaani nije kwenu au kwako?" Alijikuta akiuliza.

"Ndiyo, usiwe na wasiwasi Jan, mimi naishi kwa mjomba wangu, sijaolewa wala sina mambo mengi, nakwita kama rafiki yangu ambaye siku ile umenisaidia sana, nataka nitoe shukurani kwako, niwaonyeshe na ndugu zangu kijana aliyenisaidia, tule chakula cha mchana wote, basi, na mimi nikuonyeshe uungwana." Diana alizidi kumlainisha Jan akubali.

Amekataa mialiko ya Chala na Marco, lakini amemwalika Jan kwenye chakula cha mchana.

******************

Jan Kamili, kijana mzaliwa na Dar es Salaam, alisomea na kumaliza kidato cha nne kwenye shule ya sekondari Makumbusho.

Hakubahatika kuendelea na masomo ya juu, baada ya wazazi wake wote wawili kufariki dunia kwa ajali ya gari walipokuwa wanatoka kwenye mazishi mkoani Iringa.

Ndoto yake ya masomo ilikatishwa hapo, kwani ndugu waliobaki walikuwa wanasuasua kukubali si tu kumsomesha, bali hata kumlea yeye na wadogo zake wawili.

Wakalelewa na mama yao mdogo. Mdogo wa mama mzazi. Hakuwa na maisha mazuri, ila alikuwa na roho nzuri. Aliwalea kwa upendo mkubwa. Pamoja na hayo Jan, hakubweteka. Alianza kufanya kazi yoyote ambayo anaona inafaa. Alipopata ujira alikwenda kumpa mama yake mdogo. Mmoja wa rafiki wa baba yake aliamua kumpeleka gereji ili akapate japo ufundi ambao unamuwezesha kujitegemea baadaye.

Alijifunza kazi ya gereji, lakini pia aliendelea kufanya kazi ndogo ndogo kwa sababu gereji alikuwa halipwi.

Baada ya miezi sita alikuwa mtaalamu. Aliweza kutengeneza magari, lakini pia pikipiki. Akapendwa na watu wengi waliokuwa wakileta magari yao kwenye gereji anayofanyia kazi kwa sababu alikuwa na adabu, heshima, pia ustaarabu, lakini umri wake mdogo nao ulichangia kupendwa na kuangaliwa na jicho la huruma.

Aliweka pesa ndogo ndogo anazopata, kiasi na yeye kufungua gereji yake baada ya mwaka mmoja na nusu.

Lakini yeye alikuwa tofauti kidogo. Aliamua kuwa fundi wa mapikipiki. Kutokana na wingi wa bodaboda nyingi kwa sasa nchini aliona anatapata kazi nyingi akiwa fundi wa pikipiki badala ya magari.

Alichofanya ni kushusha bei kidogo ya matengenezo ili kuwavutia vijana wengi waendesha bodaboda kuleta kwake.

Na kweli, kutokana na uwezo wake, umaarufu wake na tabia yake ya uaminifu alipata wateja wengi. Akajulikana sana kwa jina na 'fundi mapikipiki'. Wakati baba na mama yake walipofariki, alibadilika kitabia, akawa mnyonge, asiyetaka kuongea na mtu yoyote.

Alikuwa na simanzi na majonzi yasiyopimika. Hii ilimfanya kuanza kuonewa na baadhi ya wenzake. Kunyanyaswa na kupigwa mara kwa mara. Kuna siku moja alipigwa na kijana mmoja mdogo bila sababu yoyote. Yeye ndiye aliyemchokoza na yeye ndiye aliyempiga.

Pembeni yake kulikuwa na kijana mwingine aliyekuwa akimtazama huku akitabasamu.

Akamsogelea alipokuwa akijifuta vumbi. "Unaweza kurekebisha hali hii." Aliambiwa, lakini hakuelewa.

"Huyu aliyekupiga, ukitaka unaweza kumpiga." Aliambiwa tena na yule kijana, kwa mbali ni kama alianza kumuelewa.

"Naweza kumpiga kivipi?" Aliuliza.

"Mimi nafanya mazoezi kwa master wetu Zedi, anatufundisha sanaa za mapigani, staili mbalimbali, kama unataka twende ukajiunge ujifunze. Siyo kwa ajili ya kuonea watu, ila kwa ajili ya kujilinda."

Ni siku hiyo hiyo ambaye Jan alijiunga na kambi hiyo iliyopo Kinondoni Moscow, baada ya miezi minne tu, alikuwa mahiri kwenye karate, kung fu na hata kutumia silaha za jadi kama mkuki, mshale, cheni, vijiti na fimbo. Zliwashangaza wengi, wote waliokuwa wanampiga, aliwakung'uta kwa pigo moja tu.

Alichogundua kuwa kumbe waliokuwa wanamuonea ni watu ambao hawakuwa fiti kabisa, ni kwamba jinsi alivyo hatakiwi kupigana nao, badala yake anatakiwa kupigana na watu ambao wana ujuzi na mapigano.

Hadi leo hajaacha mazoezi ya sanaa za mapigano. Ni mchezo aliotokea kuupenda sana.

Alikuwa juu ya pikipiki yake aina ya Yamaha, bomba mbili ambayo alileteshwa zawadi na mzungu mmoja rafiki yake, baada ya kumtengenezea pikipiki zake, alielekea Ubungo kwa Diana.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# WAZANZIBARI WANG'ARA SAMIA TAIFA CUP 2021

**Na Saada Akida**

ZANZIBAR imefanikiwa kung'ara katika fainali ya mashindano ya Samia Taifa Cup mwaka huu ambayo yalifikia tamati juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja wameibuka kidedea katika upande wa soka wanaume baada ya kupata ushindi wa penalti 2-1 dhidi wenzao kutoka Mara kufuatia sare ya bila kufungana kwenye dakika 90 za kawaida.

Kwa upande wa soka la wanawake, ubingwa umekwenda kwa jiji la Arusha baada ya kuibuka na ushindi wa penalti wa mabao 4-3 dhidi ya wenyeji Dar es Salaam, baada ya kukamilika kwa dakika 90 wakitoka suluhu.

Katika mchezo wa riadha, mkoa wa Kusini Unguja ulichukuwa ubingwa wa jumla kupitia kwa mwanariadha wake, Winfrida Makenji, ambaye alishinda medali mbili za dhahabu kwa kuibuka na ushindi wa kwanza shindano la mita 100 na la mita 200.

Nafasi ya pili katika mchezo huo katika umbali wa mita 100 ilikwenda kwa Haines Jackson kutoka Kusini Unguja na Kazija Hassan akitokea Kaskazini Unguja alimaliza akiwa watatu huku kwenye mbio za mita 200, Emmy Hosea kutoka Kusini Unguja alishika nafasi ya pili na nafasi ya tatu ikienda kwa Triphonia Fanuel wa Singida.

Mbio za mita 400 nafasi ya kwanza imechukuliwa na Jane Maiga huku mshindi wa pili akiwa ni Shuwena Mohamed, wote kutoka Kusini Unguja, nafasi ya tatu ikaenda kwa Sabra Makame kutoka Kaskazini Unguja wakati katika kuruka vihunzi nafasi ya pili ikiwa ni Kaskazini Unguja na bingwa ni mchezaji kutoka Tabora.

Katika mbio za 4x100m mshindi wa kwanza na wa pili wote wametoka Kusini Unguja huku nafasi ya tatu ikienda kwa mchezaji wa Tabora wakati kurusha tufe Kusini Unguja iliendelea kutawala kwa kutoa mshindi wa kwanza na wa pili na nafasi ya tatu ikichukuliwa na nyota kutoka Kusini Pemba.

Katika mchezo wa kurusha Mkuki nafasi ya kwanza imechukuliwa na Mwanaamina Hassan kutoka Kusini Unguja na Joyce Barnaba wa Dodoma amechukua nafasi ya pili wakati Tuma Makame kutoka Mjini Magharibi alishika nafasi ya tatu.

Kuruka chini imeongozwa na Baraka Barnaba kutoka Kilimanjaro, nafasi ya pili ikichukuliwa na Elias Clement wa Arusha huku mshindi wa tatu akiwa ni Rifat Salum kutoka Kaskazini Unguja.

Mgeni rasmi katika ufungaji wa mashindano hayo yaliyosimamiwa na serikali alikuwa ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo wa Zanzibar, Tabia Maulid Mwita.

# Kidunda, Katompa, Class ulingoni

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Selemani Kidunda anatarajia kuzichapa na Mkongomani Tshimanga Katompa katika pambano la 'Usiku wa Mabingwa' litakalofanyika Desemba 26, mwaka huu jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mratibu wa pambano hilo, Selemani Semunyu alisema maandalizi yanaendelea vizuri na mabondia wote wanafanya mazoezi ili kuonyesha ushindani.

Semunyu alisema pambano hilo litakuwa la raundi sita na uzito wa kilogramu 76 wakati mabondia wengine watakaopanda ulingoni siku hiyo watakuwa ni Ibrahim Class dhidi ya Israel Kamwamba kutoka Malawi huku Ismail Galiatano atachuana na Denis Mwale.

"Maandalizi kwa ajili ya mapambano yetu ya Usiku wa Mabingwa yanaendelea vizuri, mabondia wetu wanafanya mazoezi kwa ajili ya kuiweka sawa miili yao, tunaomba wadau wa ngumi wajitokeze kwa wingi siku hiyo kuona mapambano yenye viwango,"alisema Semunyu.

Mratibu huyo aliongeza anaamini wenyeji watafanya vizuri katika mapambano hayo kutokana na maandalizi ya muda mrefu waliyofanya kupitia makocha wao.

"Mabondia wa Tanzania watakaposhinda ni wazi itakuwa ni fahari, kwa sababu wataitangaza vyema nchi yetu kwa kitendo cha kuipeperusha vizuri bendera ya taifa letu," Semunyu aliongeza.




Wachezaji wa Yanga kutoka kushoto, Fiston Mayele, Djigui Diara, Saido Ntibazonkiza na Heritier Makambo wakiwa tayari kuanza safari ya kuelekea Sumbawanga kuwakabili Prisons katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Nelson Mandela. **PICHA: MTANDAO**

## JKT Tanzania FC kuongeza makali

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Mohammed Abdallah 'Bares' amesema anatarajia kufanya mabadiliko katika kikosi chake kwa kuongeza wachezaji wapya wakati huu wa dirisha dogo la usajili lililofunguliwa.

Bares aliliambia gazeti hili lengo la kuboresha kikosi chake ni kuhakikisha wanaimarika na hatimaye anafanikiwa kuirejesha timu hiyo katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Nimeona mapungufu ya kikosi changu baada ya kucheza mechi kadhaa, nitahakikisha natumia dirisha la usajili kuongeza baadhi ya wachezaji hasa katika safu ya umaliziaji," alisema Bares.

Kocha huyo alisema anatarajia kuanza mchakato wa usajili leo kwa kufanya mazungumzo na wachezaji ambao wana uwezo kutoka kwenye timu nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu watakaoachwa au ligi za chini ambao wana uzoefu.

"Ligi ya Championship ina ushindani mkubwa na tunatakiwa kupambana na kujiimarisha zaidi ikiwamo kuongeza wachezaji kwenye nafasi ya ushambuliaji ili kujiweka vizuri na kwenda kupambana kwa ajili ya kufikia malengo yetu," Bares alisema.

Alisema kikosi chake chenye pointi 19 kiko katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi ya Championship na kinaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Kengold ya Mbeya utakaochezwa Desemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo.

## Wana olimpiki sasa kuchaguana 2023

**Na Renatha Msungu DODOMA**

UCHAGUZI Mkuu wa Chama cha Wanaolimpiki Tanzania (TOA) sasa umepangwa kufanyika mwaka 2023, imeelezwa.

Awali uchaguzi wa TOA ulitarajiwa kufanyika juzi jijini hapa, lakini mchakato huo ulishindikana kwa sababu mbalimbali za kikatiba zilizobainika.

Uongozi wa TOA ulioko madarakani ambao uko chini ya Mwenyekiti, Gidemus Shahanga, Makamu Mwenyekiti, Suleiman Nyambui, Katibu Mkuu, Mwinga Mwanjala na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ni Maselina Gwandu walikuwa tayari kufanya uchaguzi huo mwingine, lakini walibanwa na katiba.

Katiba ya TOA inaelekeza chama hicho kinatakiwa kufanya Uchaguzi Mkuu ikiwa ni mwaka mmoja kabla ya kufanyika kwa Michezo ya Olimpiki, hivyo wajumbe waliamua uongozi huo uendelee kukaa madarakani.

Michezo ijayo ya Olimpiki inatarajiwa kufanyika jijini Paris mwaka 2024 wakati uongozi huo ulioko madarakani ulichaguliwa mwaka 2013 na ulitakiwa kufanya uchaguzi tangu mwaka 2017, lakini ulishindwa kufanya mchakato huo kutokana na matatizo ya kifedha.

## ZISIKUPITE

### RUDIGER ANUKIA UNITED

MANCHESTER United imeonyesha nia ya kumsajili mlinzi wa Chelsea na Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, na wana matumaini, Ralf Rangnick, anaweza kuwasaidia kuishinda Real Madrid, Paris St-Germain na Bayern Munich kwenye mchakato huo.(***Bild,via Mail***)

### RUDIGER AIGOMEA CHELSEA

ANTONIO Rudiger, ambaye mkataba wake unamalizika msimu wa joto, anapanga kuondoka Chelsea baada ya kupewa ofa ya chini ya pauni 140,000. (***FootballInsider***)

### DE JONG ATOA MSIMAMO

NYOTA anayefuatiliwa na Manchester United, Frenkie de Jong (24), angekataa fursa ya kuhamia Old Trafford kutoka Barcelona Januari kwa sababu ya hali ya hewa ya Uingereza, kulingana na baba wa kiungo huyo wa kati wa Uholanzi.(***AD,via Express***)

### HAALAND AITEGA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland (21), ameionya Barcelona kwamba hatafikiria kuhamia Nou Camp isipokuwa tu klabu hiyo kama ikifuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka ujao. (***Sport, via Star***)

### ELANGA KUMBADILI MARTIAL

MANCHESTER United ina mbadala kama mshambuliaji Mfaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 26, ataondoka huku winga wa Uswiswi, Anthony Elanga (19), akikaribia kusaini mkataba mpya baada ya kumvutia kocha mpya, Ralf Rangnick.(***Telegraph***)

### CHEEK KUTUA ROMA

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anakaribia kuishawishi klabu yake ya zamani Chelsea na ofa ya kiungo wa kati wa Uingereza, Ruben Loftus-Cheek mwenye umri wa miaka 25.(***11 Romanista,via Sun***)

### MELO ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL wanavutiwa na kiungo wa kati wa Juventus na Timu ya Taifa ya Brazil, Arthur Melo, mwenye umri wa miaka 25, pamoja na winga wa Uswisi mwenye umri wa miaka 21, Dejan Kulusevski.(***Calciomercato***)

### MYKOLENKO KUTUA DYNAMO

EVERTON iimeonyesha nia ya kumsajili beki wa kushoto wa Dynamo Kiev ya Ukraine, Vitaliy Mykolenko mwenye umri wa miaka 25, kwa dau la pauni milioni 20. (***Liverpool Echo***)

### MESLIER ATAJWA UNITED

MANCHESTER United wamemtambua, Illan Meslier wa Leeds United kama mlinda mlango bora chipukizi nchini Uingereza, lakini walipomtuma mlinda mlango, Tony Coton kumtazama Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 21, aliruhusu mabao saba huko Manchester City, Jumanne.(***Mail***)

### CENTONZE ANUKIA EVERTON

EVERTON ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England zinazomwinda mlinzi wa kulia wa Metz, Mfaransa, Fabien Centonze mwenye umri wa miaka 25.(***Football Insider***)

### AUBAMEYANG KUUZWA

KIUNGO wa zamani wa Arsenal, Emmanuel Frimpong ameitaka klabu hiyo kumuuza Pierre-Emerick Aubameyang baada ya mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Gabon mwenye umri wa miaka 32, kuvuliwa unahodha. (***Sun***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL: NGUMU KUMEZA CHELSEA KUKOSA USHINDI

## ●●● Matokeo hayo yamemchanganya kocha huyo huku akikiri walikuwa...

**LONDON England**

THOMAS Tuchel aliachwa na hasira baada ya Chelsea kukosa ushindi katika mechi yake ya Ligi Kuu England dhidi ya Everton iliyochezwa kwenye Uwanja wa Stanford Bridge juzi.

Chelsea walikosa nafasi ya kupunguza tofauti ya pointi dhidi ya vinara wa Ligi Kuu England, Manchester City wakati walipolazimishwa sare ya kufungana bao 1 - 1 na Everton.

Kikosi cha Tuchel kilianza kuongoza kwa bao la Mason Mount kabla ya Jarrad Branthwaite kusawazisha akiunganisha krosi ya Anthony Gordon na kuwawezesha Toffees kupata pointi moja.

Huo ulikuwa mchezo wa tatu kati ya sita kwa Tuchel kuacha pointi na sasa wamepitwa pointi nne na vinara na mabingwa watetezi, City.

**"Tulipata uongozi. Kama ukiangalia mechi kama hizi, tulitakiwa kupata pointi zote tatu na tulifanya jitiha da za hali ya juu sana, lakini wapinzani wetu walipata nafasi ya kusawazisha, ni ngumu kumeza," alisema Tuchel akiiambia BT Sport.**

"Nafikiri tulikosa nafasi kubwa katika kipindi cha kwanza ili kuweza kupata matokeo. kipindi cha pili hatukupata nafasi nzuri za kufunga, licha ya kutumia nguvu na akili nyingi.

"Tulipata uongozi, lakini tukashindwa kuuliza na hicho kilituweka kwenye wakati mgumu.

"Kwenye soka, mambo kama haya yanakuwa magumu sana, lakini tulikuwa hatuna namna ni kukubali tu matokeo, ingawa tulipaswa kupata ushindi wa 3-0. Kwani tulikuwa na nafasi za kutosha za kutufanya tushinde."









# TORRES ATAJWA MBADALA WA AGUERO

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona iko katika mawindo kutafuta mbadala wa mshambuliaji, Sergio Aguero (33), ambaye kwa sasa anasumbuliwa na matatizo ya moyo ambayo yamemlazimu kustaafu soka.

Ripoti zimesema Barca ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester City, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 21.

Katika kipindi cha hivi karibuni Torres amekuwa na wakati mgumu kupata muda wa kucheza chini ya Kocha, Pep Guardiola na anaweza kushawishika kuondoka.

Desemba 15, mwaka huu akiwa mbele ya viongozi na wachezaji wenzake wa Barcelona huku akitokwa na machozi, Aguero alitangaza kustaafu soka baada ya kugundulika kuwa na matatizo ya moyo na madaktari wamemshauri kuacha kucheza.

# Wanne watajwa kumrithi Cavani

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuandaa orodha fupi ya wachezaji wanne ambao wanaweza kurithi mikoba itakayoachwa na Edison Cavani kwenye kikosi cha timu hiyo, imeelezwa.


Cacani, nyota wa kimataifa wa Uruguay ni mchezaji ambaye klabu hiyo inaweza kuishia kumpoteza mara dirisha lijalo la Januari litakapofunguliwa, huku Barcelona wakionyesha nia na huduma yake.

Mchezaji huyo kwa sasa ni majeruhi, lakini amecheza mara tano pekee kwenye mechi za Ligi Kuu England msimu huu, akiwa amewachangia bao moja Mashetani Wekundu hao.

Hata hivyo, kwa mujibu wa The Express, orodha ya wachezaji wanne imeundwa ikijumuisha, Erling Braut Haaland wa Borussia Dortmund, Joao Felix wa Atletico Madrid, Alexander Isak wa Real Sociedad na Timo Werner wa Chelsea.

Wachezaji wote hao wamethibitisha kuwa bora golini wakifunga mabao katika maisha yao ya soka barani Ulaya, licha ya kuwa bado wanatamani kusalia na Cavani, klabu hiyo ina uwezekano wa kusajili mchezaji mojawapo ikiwa tu ataondoka.

United leo inatarajia kuvaana na Norwich City huku wakiwa na matarajio ya kuendelea kutopoteza mechi tangu ujio wa Ralf Rangnick.



3,781,040

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/12/2021 | 18:00 | Bristol City vs Huddersfield | 2.69 | 3.18 | 2.54 |
| 02. 18/12/2021 | 18:00 | Watford vs Crystal Palace | 2.89 | 3.34 | 2.41 |
| 03. 18/12/2021 | 20:30 | Leeds vs Arsenal | 2.97 | 3.41 | 2.32 |
| 04. 18/12/2021 | 22:45 | Cagliari vs Udinese | 3.00 | 3.29 | 2.37 |
| 05. 18/12/2021 | 23:00 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.65 | 3.00 | 2.85 |
| 06. 19/12/2021 | 15:00 | Everton vs Leicester | 2.75 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 19/12/2021 | 16:00 | Granada vs Mallorca | 2.49 | 3.14 | 2.94 |
| 08. 19/12/2021 | 16:00 | Fuenlabrada vs Real Oviedo | 2.90 | 3.05 | 2.45 |
| 09. 19/12/2021 | 17:00 | Spezia vs Empoli | 2.40 | 3.49 | 2.79 |
| 10. 19/12/2021 | 17:30 | SC Freiburg vs Bayer Leverkusen | 2.79 | 3.44 | 2.40 |
| 11. 19/12/2021 | 18:00 | Zaragoza vs Tenerife | 2.38 | 3.08 | 2.98 |
| 12. 19/12/2021 | 20:30 | Getafe vs Osasuna | 2.49 | 2.90 | 3.20 |
| 13. 19/12/2021 | 22:45 | AC Milan vs Napoli | 2.37 | 3.41 | 2.91 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 18 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 4919 | Thailand vs Singapore | 1.68 | 3.52 | 4.54 |
| 15:30 | 5213 | Middlesbrough vs Bournemouth | 2.60 | 3.14 | 2.65 |
| 16:00 | 3874 | Mtibwa Sugar vs KMC | 2.60 | 2.60 | 3.03 |
| 16:00 | 4818 | Trabzonspor vs Hatayspor | 1.79 | 3.80 | 3.95 |
| 17:00 | 2185 | Atalanta vs Roma | 1.67 | 4.18 | 4.48 |
| 17:00 | 4604 | Bohemians vs Pardubice | 1.84 | 3.76 | 4.01 |
| 17:30 | 5610 | Hoffenheim vs Monchengladbach | 2.05 | 3.82 | 3.18 |
| 18:00 | 1461 | Dundee FC vs Hearts | 3.70 | 3.36 | 1.97 |
| 18:00 | 1485 | Difaa El Jadidi vs Wydad Casablanca | 6.16 | 3.94 | 1.46 |
| 18:00 | 3027 | Forest Green vs Mansfield | 1.78 | 3.63 | 4.13 |
| 18:00 | 3866 | Warrenpoint vs Portadown FC | 2.10 | 3.61 | 2.89 |
| 18:00 | 3921 | Coleraine FC vs Crusaders Belfast | 2.84 | 3.37 | 2.22 |
| 18:00 | 3967 | Dover vs Bromley | 5.22 | 3.87 | 1.54 |
| 18:00 | 4009 | South Shields vs Witton Albion | 1.48 | 4.30 | 6.60 |
| 18:00 | 4204 | Guingamp vs Amiens | 2.14 | 3.15 | 3.44 |
| 18:00 | 4299 | Sochaux vs Nantes | 2.81 | 3.11 | 2.52 |
| 18:00 | 4782 | Ipswich vs Sunderland | 2.75 | 3.29 | 2.43 |
| 18:00 | 4920 | Kilmarnock vs Dunfermline | 1.80 | 3.43 | 4.22 |
| 18:00 | 5536 | Livingston vs Ross County | 2.32 | 3.26 | 2.96 |
| 18:00 | 5732 | Rangers vs Dundee Utd | 1.11 | 7.91 | 21.76 |
| 18:15 | 2984 | Frosinone vs Spal | 1.70 | 3.53 | 4.81 |
| 18:15 | 3135 | Real Sociedad vs Villarreal | 2.17 | 3.29 | 3.39 |
| 18:15 | 4460 | Kagera Sugar vs Simba | 6.40 | 3.25 | 1.67 |
| 18:30 | 1538 | Portimonense vs FC Arouca | 2.02 | 3.25 | 3.69 |
| 18:30 | 5573 | Fortuna Sittard vs Utrecht | 4.82 | 4.14 | 1.59 |
| 19:00 | 1452 | MTK Budapest vs Paksi FC | 2.65 | 3.66 | 2.23 |
| 19:00 | 1609 | Alanyaspor vs Adana Demirspor | 2.23 | 3.46 | 2.96 |
| 19:00 | 5168 | Galatasaray vs Basaksehir | 2.06 | 3.50 | 3.30 |
| 19:05 | 4852 | HNK Rijeka vs Istra | 1.32 | 4.99 | 6.91 |
| 20:00 | 5421 | FC Zurich vs St. Gallen | 1.89 | 3.79 | 3.54 |
| 20:00 | 5542 | Bologna vs Juventus | 3.86 | 3.47 | 1.95 |
| 20:15 | 3640 | Las Palmas UD vs Eibar | 2.22 | 3.04 | 3.33 |
| 20:15 | 5807 | The New Saints vs Penybont | 1.16 | 6.37 | 12.55 |
| 20:30 | 2058 | Azam vs Mbeya City | 1.79 | 3.00 | 4.83 |
| 20:30 | 4857 | Leeds vs Arsenal | 3.63 | 3.63 | 1.97 |
| 20:30 | 4979 | Barcelona vs Elche | 1.41 | 4.67 | 7.28 |
| 20:45 | 1671 | Sparta Rotterdam vs Vitesse Arnhem | 3.09 | 3.34 | 2.19 |
| 21:30 | 2298 | Rapid Bucuresti vs Botosani | 3.48 | 3.09 | 2.13 |
| 22:00 | 3009 | Heracles Almelo vs Groningen | 2.11 | 3.34 | 3.25 |
| 22:00 | 3622 | AZ Alkmaar vs Willem II Tilburg | 1.30 | 5.31 | 8.26 |
| 22:00 | 4535 | Dordrecht vs SBV Excelsior | 6.23 | 5.25 | 1.36 |
| 22:30 | 1946 | Hamburger SV vs Schalke 04 | 1.89 | 3.73 | 3.53 |
| 22:30 | 2389 | Notts County vs Altrincham | 1.82 | 3.56 | 3.71 |
| 22:30 | 5393 | FC Luzern vs Servette Geneva | 2.51 | 3.59 | 2.51 |
| 22:45 | 1181 | Cagliari vs Udinese | 2.95 | 3.30 | 2.39 |
| 22:45 | 4342 | KAA Gent vs St Truiden | 1.41 | 4.53 | 6.90 |
| 23:00 | 5379 | PEC Zwolle vs Twente | 3.38 | 3.28 | 2.09 |
| 23:00 | 5918 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.70 | 3.00 | 2.80 |
| 23:30 | 1961 | Gil Vicente vs Sporting Lisbon | 6.10 | 4.13 | 1.49 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# TANZANITE QUEENS KIBARUANI BURUNDI

**Na Dennis Fusi**

HAKUNA kulala. TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), inashuka ugenini Bujumbura kucheza dhidi ya wenyeji Burundi katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa wiki mbili zilizopita hapa nchini, Tanzanite Queens ilipata ushindi wa mabao 3-2.

Kocha Mkuu wa Tanzanite Queens, Bakari Shime, aliliambia gazeti hili mechi hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani kwa sababu kila timu inahitaji kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Shime alisema wachezaji wake wako tayari na mchezo huo muhimu na anaamini watapambana kuhakikisha wanapeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Alisema ameyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo wa kwanza na leo wamejiandaa kuongeza umakini ili kutowaruhusu wapinzani wao kufanya mashambulizi.

"Ni mechi ngumu kwa kila upande, ila ninamshukuru Mungu wachezaji wangu wameimarika na wataingia uwanjani wakiwa na ari mpya, tunahitaji kupata mabao ya mapema ili kujihakikishia ushindi," Shime alisema.

Tanzanite Queens ilisonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuiondoka Eritrea na katika kujiandaa na mchezo huo ilicheza mechi moja ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Uganda, ililala bao 1-0.



Nyota wa timu ya Bunge SC, Ridhiwani Kikwete (katikati), akijiandaa kuwatoka wachezaji wa Bunge la Burundi katika mechi ya mashindano ya mabunge ya Afrika Mashariki yanayoendelea jijini Arusha. Bunge SC ilishinda mabao 5-1. **PICHA: MTANDAO**

# Wabunge wagawa vifaa Arusha

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

TIMU ya soka ya wanaume ya Bunge la Tanzania imetoa msaada wa vifaa vya michezo kwa watoto wanaosakata kandanda katika kituo cha michezo cha Arusha Youth kilichopo jijini hapa.

Vifaa vya michezo vilivyotolewa ni pamoja na seti moja ya jezi, mpira pamoja na soksi ambavyo vina thamani zaidi ya Sh. milioni mbili.

Akikabidhi msaada huo, nahodha wa Bunge SC, Cosato Chumi alisema lengo la kukabidhi zawadi hizo ni kuwapa hamasa na chachu watoto hao wanaolelewa kwenye kituo hicho hasa wanaocheza mchezo wa soka.

"Sisi kama wabunge tuliungana na tukajichanga, huu ni mchango wetu wa kukuza soka nchini, kama sisi wabunge tunacheza soka kwanini watoto wasicheze," alisema Chumi.

Akipokea vifaa hivyo, nahodha wa Arusha Youth, Atwai Shaban, aliwashukuru wabunge hao na kuahidi timu yao itafanya vizuri katika mashindano yote watakayoshiriki hasa soka.

Wakati huo huo, Bunge SC imeendeleza wimbi la ushindi katika michuano ya mabunge ya Afrika Mashariki baada ya kuilaza timu ya Kenya kwa mabao 2-1.

Michezo
Jumamosi Desemba 18, 2021
Nipashe



## Tuchel: Ngumu kumeza Chelsea kukosa ushindi



Wachezaji wa timu ya soka ya wanawake ya mkoa wa Arusha, wakishangilia baada ya kukabidhiwa kikombe cha ubingwa wa michuano ya Samia Taifa Cup iliyomalizika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Arusha iliwafunga wenyeji kwa penalti 4-3 katika mchezo wa fainali. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, KAGERA KIBARUANI BARA

## •••Wekundu wa Msimbazi wazindua kampeni ya kuchangia ujenzi wa..

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam inatarajia kuendelea na kampeni ya kutetea taji hilo kwa kuwakabili Kagera Sugar katika mechi ya raundi ya tisa itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Simba itaingia uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya sare ya bila kufungana dhidi ya watani wake wa jadi Yanga iliyochezwa Jumamosi iliyopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Ofisa Habari wa Simba, Ally Shatry 'Chico' alisema wanatarajia mechi hiyo itakuwa ngumu kutokana na historia ya timu hizo mbili kila zinapokutana, hasa kwenye Uwanja wa Kaitaba.

"Haitakuwa mechi nyepesi, hasa Kagera Sugar huwa wanakuwa wagumu wanapocheza na sisi kwenye uwanja wao wa nyumbani, lakini kocha wetu Pablo (Franco), anaamini mechi nyingi za mikoani huwa ni ngumu na zinatakiwa maandalizi ya ziada," alisema Chico.

Aliongeza wamejiandaa kuingia na mfumo tofauti katika mchezo huo ambao utaendana na mazingira ya wapinzani wao watakavyokuwa. "Lakini tukumbuke timu hizi mara nyingi zikicheza na timu kubwa huwa zinapambana kweli kweli, lakini kwa sababu sisi ni mabingwa watetezi lazima tuonyeshe ubingwa wetu, sisi kila mechi ni ngumu na ni sawa na fainali," Chico alisema.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, aliliambia gazeti hili kikosi chake kitaingia uwanjani huku wakiipa heshima Simba na wamepanga kutumia mifumo mbalimbali kulingana na mazingira ya mechi yenyewe.

"Ni ukweli usiopingika kuwa Simba ni timu kubwa, siyo Tanzania tu, bali Afrika nzima kwa sasa. Inailetea nchi sifa, ina historia nzuri kwa hiyo tunapoingia ni lazima tuipe heshima na si kama tunakwenda kucheza na timu nyingine ya kawaida. Tunaingia na mfumo wetu tulioupanga, lakini hatutoung'ang'ania, tutakuwa tunabadilika kutokana na mazingira yatakavyokuwa," Baraza alisema.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakuwa ni kati ya Azam FC ambayo itawakaribisha Mbeya City kwenye Uwanja wa Azam Complex, uliopo Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Kocha wa makipa wa Azam FC, Iddy Abubakar alisema mechi hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani kwa sababu ya historia ya ushindani kila timu hizo mbili zitakapokutana.

Kocha huyo alisema mara nyingi wanapokutana na Mbeya City iwe nyumbani au ugenini, mchezo huwa na ushindani mkubwa kutokana kwa sababu kila timu kucheza kiufundi zaidi.

"Mechi itakuwa na ushindani zaidi na ugumu kwa kila upande, kikubwa tumejiandaa vizuri ili kuondoka na pointi tatu katika mchezo wetu dhidi ya Mbeya City," alisema Iddy.

Nahodha wa Azam FC, Sospeter Bajana alisema wamejiandaa vizuri kwenda kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo na mabadiliko ya benchi la ufundi yaliyotokea hayawezi kuathiri kikosi chao.

Kocha Msaidizi wa Mbeya City, Mathias Wandiba, alisema kuelekea mechi hiyo wamefanya maandalizi mazuri na watashuka dimbani wakiwa imara kuhakikisha wanapata pointi muhimu katika mchezo huo.

"Hatuna presha tumejiandaa vizuri na tunaenda kutafuta pointi muhimu, Azam FC ni timu kubwa na inawachezaji wazuri lakini tunaenda kupambana kutafuta matokeo chanya," alisema Wandiba.

Alisema kiufundi wako vizuri ingawa watawakosa wachezaji wetu ni George Sangija, David Mwasa na Pato Ngonyani ambao ni majeruhi. Katika hatua nyingine, uongozi wa Simba umetangaza rasmi kampeni ya kuchangia a ujenzi wa uwanja wa kisasa klabu hiyo utakaojengwa hapa jijini.

Kampeni hiyo imezinduliwa na Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu ikiwa ni siku chache zimepita tangu Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez kuzuiwa kuingia uwanjani katika mechi ya watani wa jadi iliyochezwa Jumamosi iliyopita.

Kampeni hiyo itaitwa 'Simba Yetu, Uwanja Wetu.

## Yanga kufanya usajili kimkakati

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI uongozi wa Yanga ukisema usajili wao katika dirisha dogo lililofunguliwa utafanyika 'kimkakati', kikosi cha timu hiyo kimeshatua salama Sumbawanga kwa ajili ya mchezo wake wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya 'Maafande' wa Prisons utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini humo.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliliambia gazeti hili klabu hiyo itafanya mchakato huo kwa kuangalia nafasi wanazotakiwa kujaza kutokana na mapengo ya wachezaji ambao ni majeruhi.

Bumbuli alisema kamwe hawatafanya usajili wa wachezaji wapya kwa 'kukurupuka' lakini pia wakiwa na mpango wa kuwaongezea mikataba nyota wao ambao bado wako kwenye mipango ya kocha.

"Hatutafanya usajili mkubwa, tuna majeruhi ambao ni Kibwana Shomari, Yusuph Athumani, Fiston Mayele na Yacouba Songne ambaye kwa muda mrefu yupo nje, hivyo usajili wetu utazingatia maeneo hayo ya kuziba nafasi hizo ili tusitetereke. Kwa maana hiyo tutasajili straika ili kuwasaidia Heritier Makambo na Mayele, pia tunataka kusajili kiungo mchezeshaji, ni usajili wa kimkakati," alisema Bumbuli.

Aliongeza pia Yanga inatarajia kutoa wachezaji wengine kwa mkopo baada ya taratibu zote kukamilika na klabu nyingine zitakazowahitaji.

"Yanga ni klabu kubwa, itakuwa inahusishwa na wachezaji wengi kama tulivyoanza kuona kwenye mitandao na vyanzo vingine, lakini hatujatangaza jina la mchezaji yoyote yule, kila kitu ambacho tutakifanya tutakiweka wazi, kuhusu usajili, kuongeza wachezaji mikataba na kuwatoa kwa mkopo tutatangaza ifikapo Desemba 30 au 31, hivi sasa mawazo yetu tumeyaelekeza kwenye mechi zilizo mbele yetu," Bumbuli alisema.

Tayari Yanga imeanza kuhusishwa na wachezaji Salum Aboubakar 'Sure Boy' wa Azam FC, Jean-Marc Makusu, straika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), na winga, Denis Nkane wa Biashara United.

Yanga ndio vinara wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara wakiwa na pointi 20 wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba wenye pointi 18.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >